Thomas Schirrmacher

Sheria au Roho?

RVB International

1	Thomas Schirrmacher:	GOD Wants You to Learn Labor and Love
2	Thomas Schirrmacher:	Legends About the Galileo-Affair
3	Thomas Schirrmacher:	World Mission – Heart of Christianity
4	Thomas Schirrmacher:	Law or Spirit – an alternative View of Galatians
5	Thomas Schirrmacher:	Human Rights Threatened in Europe
6	Thomas Schirrmacher:	Be keen to get going – William Carey's Theology
7	Thomas Schirrmacher:	Love is the Fulfillment of the Law
8	Thomas Schirrmacher:	Studies in Church Leadership
9	Monte Wilson:	The Most Important Rule for Living
10	Monte Wilson:	Principles of Success in Business
11	Th. Schirrmacher (Ed.):	A Life of Transformation – From Politician to Good Samaritan – A Festschrift for Colonel Doner
12	Thomas Schirrmacher	DIOS Quiere Que tu Aprendas, Trabajes y Ames
13	Christine Schirrmacher	La Vision Islamica de Importantes Enseñanzas Cristianas
14	Thomas Schirrmacher	Sheria au Roho
15	Thomas Schirrmacher	Upendo ni Utimilifu wa Sheria
16	Thomas Schirrmacher	Mateso ya Wakristo Yanatuhusu Sisi Sote
17	Monte Wilson	Sheria Muhimu Zaidi katika Kuishi

Thomas Schirrmacher

Sheria au Roho?

Mtazamo Mbadala kwa Wagalatia

Kimetafsiriwa na Emmanuel E. Buganga

RVB
International

Die Deutsche Bibliothek – CIP

Bibliografische Information Der Deutschen Bibliothek

Die Deutsche Bibliothek verzeichnet diese Publikation in der Deutschen Nationalbibliografie; detaillierte bibliografische Daten sind im Internet über http://dnb.ddb.de abrufbar.

Bibliographic information published by Die Deutsche Bibliothek

Die Deutsche Bibliothek lists this publication in the Deutsche Nationalbibliografie; detailed bibliographic data are available in the Internet at http://dnb.ddb.de

ISBN 978-3-928936-23-1

© Copyright 2001, 2007 by
Reformatorischer Verlag Beese
www.rvbeese.de / info@rvbeese.de
Printed in Germany

ISBN 9976 906 93 5

© Kwa Toleo la Kiswahili, 2007
2nd edition 2009
Trans-Africa Swahili Christian Ministries
P.O. Box 772, Mwanza, Tanzania
Toleo la Kwanza, 2007 Nakala 5,000

Kimetolewa na Inland Publishers, S.L.P. 125, Mwanza, Tanzania
E-mail: ipublishers@hotmail.com

Maandiko Matakatifu:
The Holy Bible in Kiswahili
Union Version, 1994

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kurudufu au kutoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini ya Trans-Africa Swahili Christian Ministries, Idara ya Maandiko.

Kimepigwa Chapa na: Inland Press, P.O. Box 125, Mwanza, Tanzania
(East Africa) TEL. +255 28 2560175 inlandpress@yahoo.com

YALIYOMO

Utangulizi 8

Shukrani. 10

Maeleza na Maandiko. 11

1. Makundi mawili katika Kanisa la Galatia. 13

2. Wagalatia 1:1-5: Hakuna injili ya mtu, kama Wasio-sheria Walivyoamini. 18

3. Wagalatia 1:6-10: Paulo hahubiri injili nyingine kama vile kundi la Wana-uhuru lilivyodai. 20

4. Wagalatia 1:10-24 na 2:1-14: Paulo hakupokea injili yake kutoka kwa watu, kama kundi la Wana-uhuru lilivyodai. 21

5. Wagalatia 2:15-17: Upendeleo wa Wayahudi unapinga kundi la Wasio-sheria. 25

6. Wagalatia 3:1-29: Agano la Ahadi kwa Ibrahimu ni kuu kuliko Sheria, lakini halifuti uhalali wa Sheria. 27

7. Wagalatia 3:8-14: Je, Sheria inajipinga yenyewe?. 32

8. Wagalatia 3:13-14: Mataifa pia wanakabiliwa na hukumu Chini ya Sheria. 36

9. Wagalatia 3:19-21: Malaika na Sheria. 38

10. Wagalatia 3:24: Sheria kama Kiongozi. 40

11. Wagalatia 4:1-20: Mataifa pia wanawekwa huru kutoka katika kawaida za kwanza za dunia. 42

12. Wagalatia 5:1: Sheria ya Uhuru 45

13 Mapitio: Juu ya Tofauti kati ya Sheria ya Maadili na Sheria ya Maadhimisho. 47

14. Wagalatia 5:6 na 6:15: Sheria ya Maadhimisho katika Waraka kwa Wagalatia. 50

15. Wagalatia 5:7-12: Kujipenyeza kwa ukosa-sheria wa kipagani, kwa kiwango cha kujikata binafsi. 52

16. Wagalatia 5:11: 6:12 Sababu ya mateso. 55

17. Wagalatia 5:13-26: Uhuru danganyifu wa wasio-sheria. 57

18. Wagalatia 6:1-10: Paulo anawasihi Wasio-sheria kuchukua mizigo ya wengine na kufanya mema. 61

19. Wagalatia 6:2: Sheria ya Kristo inawafunga pia wasio-sheria. 63

20. Wagalatia 6:11-18: Kutokuwa sawa kwa kundi la Washika-sheria. 67

21. Mapitio: Imani za ushika-sheria. 68

Kiambatisho: Ulinganifu na kitabu cha Warumi

Rejea za Nukuu

Mwandishi

Mwandishi

Tabaruku kwa Kumbukumbu ya Wilhelm Lütgert (1867-1938)

“Je! Nimekuwa adui yenu kwa sababu nawaambia yaliyo kweli?”

Paulo, katika Wagalatia 4:16, mwaka 49 BK.

“Kwa kuwa Kristo ametuweka huru kutoka katika laana ya Sheria, sio kuacha kuitii”

(Martin Luther, 1532, Mahubiri juu ya Wagalatia 3:23-24)

“Uhuru Kristo atoao, sio ukosa-sheria wa kipagani.”

(Wilhelm Lütgert, katika Komentari yake ya Wagalatia, 1919)

UTANGULIZI

Hoja: Waraka kwa Wagalatia haupaswi kueleweka kama upinzani kwa dini ya Kiyahudi na Ushika-sheria tu.

Waraka wa Paulo kwa Wagalatia una maneno 2,300[1], ni mfupi zaidi kuliko kitabu cha Warumi au nyaraka za Wakorintho, pia unashughulikia dhamira chache kuliko nyaraka nyingine; ingawa matatizo ya waandikiwa wa nyaraka hizo yana mengi yanayofanana. Hata hivyo, Wagalatia ni waraka wenye umoja zaidi katika dhamira yake kuu, kuliko nyaraka ndefu za Paulo, zaidi ya Waefeso ambao ni wenye urefu ulio sawa, na zaidi ya zile nyaraka fupi zaidi[3]. Kwa kweli, unahusika na uhusiano wa Wakristo na Agano la Kale tu.

Wakristo wengi huamini kwamba Waraka kwa Wagalatia uliandikwa kupinga Sheria ya Agano la Kale na kupinga matumizi yake katika Kanisa la Agano Jipya. Wanadai kwamba waamini lazima waishi chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu tu na sio kwa kulingana na amri zilizotolewa na Mungu chini ya Agano la Kale.

Hata hivyo, mtazamo huu tatanishi wa waraka wa Wagalatia kuwa uko kinyume na Uyahudi au Agano la Kale haukitendei haki kitabu hiki. Kama afanyavyo katika Warumi[3], mara nyingi Paulo anaongea vizuri juu ya Sheria na Agano la Kale katika Wagalatia, kuliko kuikataa kabisa katika Wagalatia. Anapinga 'Wana-uhuru' na 'Wana-Roho' (Wakristo waliomshikilia Roho Mtakatifu kama leseni ya zinaa na uchafu), na kwa uwazi kabisa anaufanya waraka huu kushughulika na hatari za Ushika-sheria tu.

Bila ubishi, Paulo anaonya dhidi ya jitihada za kuhesabiwa haki kwa matendo. Hakuna hata mmoja awezaye kuokolewa kwa matendo ya Sheria (Gal.2:16), ama sivyo Kristo angekuwa amesulubiwa bure (2:21). Hakuna hata mmoja ampokeaye Roho wa Mungu kwa njia ya Sheria (3:2), na wala Sheria haiji kwa imani (3:12); hivyo basi Kristo alipaswa kufa ili kutukomboa sisi kutoka katika laana ya Sheria (3:13). Yeyote ajaribuye kuhesabiwa haki kwa Sheria (5:4) ni lazima ashike amri zake kikamilifu (5:3) na wala sio baadhi ya sehemu tu kama vile tohara (6:13).

Katika somo hili nitadhihirisha hoja tatu:

1) **Kwa kweli, onyo dhidi ya Sheria ni onyo dhidi ya matumizi mabaya ya Sheria kama njia ya wokovu na dhidi ya kuwalazimisha waamini wa Mataifa kujiweka chini ya sheria za maadhimisho (kwa mfano, tohara),** lakini sio onyo dhidi ya matumizi sahihi ya viwango vya Mungu juu ya Mema na Mabaya.

2) **Kanisa la Galatia lilikuwa na makundi mawili yaliyopingana vikali, ambayo Paulo anayapinga yote mawili kwa nguvu sawa.** Kundi moja lilitumia Sheria vibaya kama njia ya wokovu na lilitaka kulazimisha sheria za maadhimisho za Agano la Kale (kama vile tohara) kwa Wakristo wa Mataifa. Kundi jingine lilitupilia mbali kabisa Sheria ya Agano la Kale (kama vile Amri Kumi) na lilijaribu kuhalalisha zinaa yao kwa kudai kuishi 'katika Roho' kwa kulingana na mafundisho ya 'uhuru' katika Kristo.

3) **Paulo anashambulia Ushika-sheria wa kundi moja na Ukosa-sheria wa kundi jingine,** hivyo anahukumu matumizi mabaya ya Sheria kama njia ya wokovu na pia anapinga ukataaji wa sheria za maadili za Agano la Kale. Kwa Paulo, uhuru mbali na Sheria ilimaanisha uhuru kutoka katika laana yake na uwekwaji huru wa Wakristo wa Mataifa kutoka katika maadhimisho yake. Uhuru huu hautupilii mbali amri za Mungu bali humsaidia mwamini kuonesha upendo wake ambao [Wana-uhuru] wanaufasili na kuuhitaji. Wilhelm Lütgert anaelezea kwa ufupi na uwazi: "Uhuru Kristo atoao, sio ukosa-sheria wa kipagani."[4]

Shukrani

Kwa maoni yangu, maelezo bora ya Waraka kwa Wagalatia yalitolewa na Wilhelm Lütgert (1867-1938)[5] mnamo mwaka 1919[6]. Tafsiri yake, ambayo inaelekezwa dhidi ya madai kuwa waraka kwa Wagalatia unaikataa kabisa Sheria ya Agano la Kale; inafanya msingi wa kitabu changu, ingawa mawazo yangu yote si yale yanayopatikana katika kitabu chake[7]. Nimekiweka wakfu kitabu changu kwake kwa sababu hii.

Mawazo ya Lütgert yalirithiwa na James Hardy Ropes[8] mnamo mwaka 1919 na Frederic R. Crownfield[9] mnamo mwaka 1945[10]. Kipekee, Mlutheri Mswideni, Ragnar Bring, ameonesha kwenye komentari yake ya Wagalatia[11] kwamba Paulo hakuipinga sheria ya maadili.

Mbali na Lütgert, mara nyingi ninarejea kwenye vitabu vyangu vya Warumi na juu ya Elimu-maadili[12], kwa kuwa vinashughulikia mambo mengi kutoka katika mtazamo wa Maandiko Matakatifu kwa jumla; ambayo hapa yanahusishwa na mtazamo wa Wagalatia. Marudio ya matamko juu ya mambo haya kwenye vitabu vyangu hayawezi daima kuepukwa hususani katika mapitio ya kimsingi.

Sura ambazo hazishughuliki moja kwa moja na Wagalatia lakini zinatoa historia muhimu, au zinawasilisha uwiano wa ujumbe wa kitabu; zimeoneshwa kama mapitio, zinapatikana kwenye kitabu changu na ni muhimu kwa kuielewa hoja yangu.

Kila sura itatambulishwa kwa ufupisho wa hoja na kifungu husika cha Wagalatia (Swahili Union Version). Sitashughulika na vifungu vifuatavyo dhidi ya kuhesabiwa haki kwa matendo: Wagalatia 2:18-21; 4:21-31; 5:2-5.

Kazi hii haikusudiwi kuwa komentari ya Waraka kwa Wagalatia[13], bali wasilisho la fasili mbadala. Itachunguza mwelekeo wa Paulo kwa mambo ya ushika-sheria na ukosa-sheria kutoka katika msimamo wa kimaadili. Kwa sababu hii, baadhi ya sehemu zitajadiliwa kikamilifu, na nyingine zitatajwa tu.

Ningependa kutoa shukrani zangu kwa mke wangu, Christina; kwa mama yangu, Ingeborg Schirrmacher; kwa dada yangu, Ingrid von Torklus; kwa rafiki na mwanafunzi mwenzangu wa zamani, Titus Vogt; na kwa Cambron Teupe kutoka katika kanisa letu la mtaa kwa usomaji thibitifu.

Cambron Teupe amekwisha tafsiri dazani nyingi za insha zangu kwa Kiingereza na tena amefanya kazi ya kushangaza kwenye kitabu hiki!

Maelezo na Maandiko

Nukuu za Maandiko zimechukuliwa kutoka katika The Holy Bible in Kiswahili: Union Version (1994). Vifungu vyenye mlazo katika tafsiri hii huonesha mabadiliko yaliyofanywa na mwandishi, kama haikudokezwa vinginevyo.

Vifupisho vya majina ya vitabu vitatumika kwa vitabu vifuatavyo:

Daniel P. Fuller, The Unity of the Bible. Unfolding God's Plan for Humanity, (Grand Rapids: Zondervan, 1992): Fuller, Unity.

Wihelm Lütgert, Gesetz und Geist: Eine Untersuchung zur Vorgeschichte des *Galaterbriefes, Beiträge zur Forderung christlicher Theologie 22, no. 6, (Gutersloh, Germany: Bertelsmann, 1919) Lütgert, Gesetz und Geist.*

Wilhelm Lütgert, Der Römerbrief als historisches Phänomen, Beiträge zur Forderung christlicher Theologie 7, no. 2 (Gutersloh, Germany: Bertelsmann, 1913): Lütgert, *Römerbrief.*

Thomas Schirrmacher, Ethik, 2 vols. (Neuhausen, Germany: Hanssler, 1994): Schirrmacher, Ethik 1+2.

Thomas Schirrmacher, Paulus im Kampf gegen den Schleier: Eine alternative Sicht von. *1. Korinther 11, 2-16, Biblica et symbiotica 4, (Bonn, Germany:Verlag fur Kultur und Wissenschaft, 1993): Schirrmacher., Paulus im Kampf.*

Thomas Schirrmacher, Der Römerbrief, 2 vols. (Neuhausen, Germany: Hanssler, 1994): Schirrmacher, Römerbrief 1+2.

MAKUNDI MAWILI KATIKA KANISA LA GALATIA

Hoja: Kulikuwa na makundi mawili pinzani katika kanisa la Galatia. Kundi la Washika-sheria lilifundisha kwamba utii wa Sheria ni muhimu kwa wokovu; kundi la Wakosa-sheria liliikataa Sheria kwa ujumla.

C.S. Lewis anaandika vema:

> "Shetani…daima hupeleka makosa duniani kwa pea - pea zilizo tofauti. Na daima hututia moyo kutumia muda mwingi kufikiri lipi ni baya sana. Hata hivyo, unadhani ni kwa nini? Anaegemea kwenye kosa usilolipenda zaidi ili kukuvuta taratibu uelekee kwenye upande upande mwingine ulio tofauti. Lakini tusijiache tukapumbazika. Tunapaswa kuyaelekeza macho yetu kwenye lengo na kwenda wima tukipita katikati ya makosa yote mawili".[14]

Vilevile, kuna maandiko mengi yanayozungumzia makosa mawili yenye kuchanganya kwa wakati mmoja; kwa mfano, Kanisa la Korintho liligawanyika katika mitazamo yake karibu katika kila jambo.[15] Baadhi yao walikula nyama iliyokuwa imekwishatolewa dhabihu kwa sanamu, wakati wengine ili waweze kula nyama hiyo, walishiriki hata katika utoaji wa dhabihu. Baadhi waliamini juu ya uhuru wa kimapenzi, wengine walikana tendo la kujamiiana hata katika ndoa. Kwa ujumla ni mara chache Paulo anakubaliana na kila upande, lakini anakemea makundi yote mawili sawia kwa kuwa hakuna upande unaolingana na viwango vya Mungu.

Watoa hoja (Makomenteta) wengi hudhani kwamba kanisa la Galatia lilimfikishia Paulo wazo moja la kizushi, na kwamba somo moja tu la waraka kwa Wagalatia ni onyo dhidi ya ushika-sheria, kugeukia tena tohara na imani kwamba utii kwa sheria waweza kumhesabia Mtu haki mbele za Mungu: "Mmetengwa na Kristo, ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria, mmeanguka na kutoka katika hali ya neema" (Gal.5:4).

Kuna hoja kadhaa kinyume na mtazamo huu:

1) Kitabu chenyewe cha Wagalatia kinataja mgawanyiko ndani ya kanisa. Mfano wa wazi kabisa ni Wagalatia 5:15: "Lakini mkiumana na kulana, angalieni msije mkaangamizana"[16]. Ukihukumu kutoka kwenye muktadha, mstari huu waweza kuelezea kwa taabu migogoro baina ya watu, bali kwa wazi unaelezea kutokukubaliana

juu ya kazi ya Sheria ya Agano la Kale. Hili pia linakubalika kwa Wagalatia 5:26: “Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana”.

2) Wakati Kanisa lilijumuisha zaidi waamini wa Mataifa, Paulo anazungumzia mambo halisi ya Wakristo wa Kiyahudi. Hii inaashiria kuwa alikuwa anashughulikia uzushi wa Wayahudi na wa Mataifa kwa ujumla.[17]

Haiwezekani kabisa kuwa kanisa la Mataifa lingejitoa kikamilifu kujaribu kuwa la namna ya Kiyahudi pasipo sababu. Mgawanyiko miongoni mwa waamini wa Mataifa waliofuata kosa la Kiyahudi, na wengine waliowakataa kwa kutumia fikra zisizo za kibiblia yanaelezea utajaji wa daima wa Paulo juu ya migogoro.[18]

Waamini wa Kiyahudi na wa Mataifa walitofautiana juu ya suala la tohara, kwa kuwa ni wale wasio Wayahudi tu wangelazimishwa kutahiriwa. Wagalatia 5:6 na 6:15 husema juu ya kiburi cha kundi moja katika ‘tohara’ yake na kiburi cha jingine katika ‘kutokutahiriwa’ kwake.[19]

3) Kitabu cha Wagalatia mara nyingi kinazungumzia kundi moja tu la kanisa, mfano, kama ilivyo katika Wagalatia 4:21, “Niambieni, ninyi mnaotaka kuwa chini ya sheria, je! Hamwisikii sheria?”. Paulo anaongea na wale washiriki wa kanisa walioishi kwa kulingana na Sheria tu, jambo ambalo linaonesha kuwa si wote waliokubaliana juu ya jambo hili.[20] Mfano mwingine ni Wagalatia 5:4, “Mmetengwa na Kristo, ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria, mmeanguka na kutoka katika hali ya neema”, ambao unazungumza na washiriki waliotafuta kuhesabiwa haki chini ya Sheria. Ingawa kwa ujumla anakataa wazo la kambi mbili katika kanisa la Galatia, [21] Theodor Zahn anaamini kwamba, hapa Paulo anazungumza na sehemu tu ya kanisa.[22]

Wagalatia 6:1 pia inazungumzia sehemu tu ya ushirika, wakati Paulo aandikapo, “ninyi mlio wa Roho”[23] au (“Ninyi mnaojiona kuwa wa kiroho zaidi”). Hapa, mtume anazungumza na wale ambao waliamini kuwa wao wenyewe ni wa kiroho zaidi kuliko wengine. Theodor Zahn aliwaita watu hawa ‘Wana-roho.[24] Anawalinganisha na ‘wenye nguvu’ wa Warumi 14 na 15, waliojishikilia wenyewe kama Wakristo bora zaidi ya waamini ‘dhaifu’ wa Kiyahudi. [25]

4) Hakuna kutokukubaliana juu ya ukweli kuwa makanisa yote ya Galatia yalijumuisha Wakristo waliodanganywa na dini ya kiyahudi

ili kuishika sheria ya Agano la Kale, walau kwa sehemu. Vifungu vionyavyo dhidi ya zinaa na vinavyokataa Sheria, vyote kwa pamoja vinathibitisha kwamba kulikuwa na kundi la pili ndani ya kanisa. Kama ilivyo katika nyaraka nyingine, Paulo anapinga tafsiri isiyo sahihi ya uhuru mbali na Sheria: “Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili” (Gal.5:13-14). Uhuru huu usioongozwa ni vigumu kuweza kuwa ulianzishwa na Wana-Uyahudi [26], bali unahitaji kuwapo kwa maadui wa Sheria.

5) Paulo daima anawapinga waamini hawa wa kiliberali kwa mtazamo chanya (mtazamo unaokubaliana na jambo au unaojenga) wa Sheria. Hili ni wazi zaidi katika jibu lake kwa swali, “Basi, je! Torati haipatani na ahadi za Mungu? Hasha!” (Gal.5:21). Badala yake, Sheria ni “Kiongozi” (Gal.3:24), ambapo kwenye maandiko ni cheo cha heshima.

Kwa hiyo, Sheria si kinyume cha ahadi, bali ina lengo muhimu la kielimu na inatutambulisha kwa Kristo (Gal.3:21-24), sifa isiyoelekezwa kwa mtu awaye yote au kitu chochote. Sheria inatimilizwa katika upendo (Gal.5:14), inapingana na matendo ya giza (Gal.5:19), na kamwe si matunda ya Roho

Maelezo ya Histlahi za Kitheolojia Zilizotumika kwa Makundi Mawili
Washika - Sheria
Wana -uyahudi (usiwachanganye na Wayahudi) -Hawa ni Wakristo, wengi wao wa Kiyahudi, waliotaka kuwalazimisha waamini wa Mataifa kushika maadhimisho ya sheria ya Agano la Kale, au waliozingatia utii kwa Sheria kama kitu muhimu kwa wokovu
Wana -sheria [27] (au Wanoministi, kutoka katika Kigriki "nomos" =Sheria). Wakristo, wengi wao wa kiyahudi, wliotaka kuwalazimisha waamini wa Mataifa kushika maadhimisho ya Sheria ya Agano la Kale, au waliozingatia utii kwa Sheria kama kitu muhimu kwa wokovu.
Wasio -Sheria
Wapinga wana -uyahudi ('anti' -Judaists, Kigriki anti = kinyume, kupingana na Judaist = wana-uyahudi)- Wapinzani wa wana -uyahudi.
Wana -roho (pneumaticists, Kigriki 'Pneuma'= roho) -Wakristo, yawezekana wa Mataifa waliokataa Sheria ya Agano la Kale na kutegemea moja kwa moja mafunuo ya Roho Mtakatifu.
Wana -Uhuru (Libertines, Kilatini 'libertas' = uhuru) - Wakristo, yawezekana wengi wao ni wa Mataifa, waliokataa aina zote za Sheria, walioamini katika uhuru kamili wa maadili na walioishi kwa kutenda uzinzi.
Wapinga sheria[28] (Antinomians) - Wakristo, wengi wao wa Mataifa, ambao waliikataa kabisa sheria ya maadili.

(Gal.5:32). Kwa sababu hii, hutimiza “sheria ya Kristo” (Gal.6:2). Paulo hakuhitaji kulinda Sheria kwa Wana-uyahudi, bali ilikuwa ni muhimu kuelezea thamani na umuhimu wake kwa Wana-uhuru.

Kama ilivyo mara nyingi kwenye nyaraka zake[29], Paulo ni lazima azungumze na wapinzani wake washikao itikadi kali zaidi. Katika waraka kwa Wagalatia watu hawa ni Wakristo wa Kiyahudi, waliotarajiwa kuokolewa kwa Sheria, kipekee, kwa taratibu za maadhimisho; na kwa upande mwingine, waamini wa Mataifa waliotaka kutupilia mbali, tena kimoja sheria ya maadili ya Mungu.

WAGALATIA 1:1-5 : HAKUNA INJILI YA MTU, KAMA WASIO-SHERIA WALIVYOAMINI

Hoja: Mwanzoni kabisa mwa waraka wake, Paulo anakanusha mashtaka ya Wana-roho kwamba Injili yake ilikuwa ya Kiyahudi zaidi kutokana na asili yake ya Ukristo wa Kiyahudi. Katika baraka zake, anadokeza kwamba mwamini hawezi kamwe kuhalalisha uovu kwa sababu za utawa.

Wagalatia 1:1-5: “Paulo, mtume, (si mtume wa wanadamu, wala kutumwa na mwanadamu, bali na Yesu Kristo, na Mungu Baba aliyemfufua kutoka kwa wafu), na ndugu wote walio pamoja nami, kwa makanisa ya Galatia; Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba, na kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa, kama alivyopenda Mungu, Baba yetu. Utukufu una yeye milele na milele, Amina.”

Kuanzia mstari wa kwanza kabisa, Paulo anarudia kukanusha mashtaka kwamba alipokea Injili kutoka kwa watu, wazo ambalo yawezekana lilikuja sio kutoka kwa Wana-uyahudi, bali kutoka kwa Wana-roho, ambao waliyaweka mafundisho ya Paulo kuwa yalikuwa yameanzishwa na uongozi wa Kikristo wa Kiyahudi wa huko Yerusalemu, hivyo basi alikuwa hajajitenga na torati kikamilifu, bali alitetea uhalali wa matakwa yake ya maadili.

Salamu na baraka zinazofuata (Gal.1:3-5) zinajumuisha pia hoja chokozi dhidi ya Wana-roho, “…ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa, kama alivyopenda Mungu, Baba yetu (mst.4). Kristo hakutukomboa kwa ajili ya ukombozi, bali kwa ajili ya utakaso wa mwamini, ambaye anapaswa kuishi kwa kulingana na mapenzi ya Mungu, na sio kwa kulingana na mapenzi yake mwenyewe.

(Mapitio) Wakiulizwa ni kwa ajili ya nani Kristo alikufa msalabani, Wakristo wengi hujikuta wakijibu, “Kwa ajili ya watu wote!” Hata hivyo, maandiko mengi yanayojishughulisha na swali hili, huongea wazi juu ya kifo chake au ujio wake kwa “kanisa” au kwa ajili “yetu” (rejea Mat. 1:21; Yoh. 10:15; Rum. 8:4, 31-33; 2 Kor. 5:21, Gal. 1:3-5; Efe.5:25; 1 Yoh. 4:10, linganisha na Efe. 1:4, Yoh. 17:19)[30]. Paulo anasisitiza hili pekee

katika Wagalatia. Kwa mfano, anasema, “Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba, na kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa, kama alivyopenda Mungu, Baba yetu” (Gal.1:3-4). Ni sawa na Wagalatia 3:13, “Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu…”. Katika Wagalatia 2:20, anazungumza juu yake mwenyewe, “Nimesulibiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.”(mlazo ni wa mwandishi).

WAGALATIA 1:6-10 : PAULO HAHUBIRI INJILI NYINGINE KAMA VILE WANA-UHURU WALIVYODAI

Hoja: Badala ya kuachana na dini ya Kiyahudi na Torati kwa pamoja,Wana-uhuru walimlaumu Paulo kwa kufundisha Injili nyingine na ya uongo, kwa sababu alishikilia chembechembe za Kiyahudi, Injili iliyoibuka kutokana na tofauti za kibinadamu baina yake na mitume huko Yerusalemu

Wagalatia 1:6-10: “Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe.

Maana, sasa je! Ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo.”

Katika fungu hili tunapata mawazo kwamba Paulo alikuwa akihubiri injili tofauti.[31] Angeweza kurejea kwa wainjilisti wengine au kwa malaika, badala yake anayachukua mashtaka kwamba anaifanyia uzinzi Injili ya kweli bila kuwajali wengine. Hata kama ilikuwa hivyo, ujumbe aliouhubiri kwanza ungekuwa injili ya kweli, na chochote ambacho angeweza kusema bila kuwajali wapinzani wake katika Galatia ungekuwa ni uzinzi. Waziwazi, kundi la Wana-roho lilikuwa limepokea mafunuo kutoka kwa ‘malaika’, ambao uliwaruhusu kuwa wasio-sheria, wakichafua Ukristo. Paulo analaani mafunuo haya, kama alivyofanya kwa mafundisho ya wale waliotarajia kuokolewa kwa kushika Sheria na sio kwa imani katika dhabihu ya Yesu Kristo.

> “Mashtaka ya ‘Wana-roho’ ndio msingi wa utetezi na maswali ya Wagalatia 1:10, ‘Maana, sasa je! Ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu?’ Wilhelm Lütgert anaeleza wazo hili ambalo baadaye tutalizingatia kwa kina wakati tuchunguzapo Wagalatia 5:11 na 6:12: “Ikiwa bado alihubiri tohara, kama walivyodai wapinzani wake kuwa alifanya hivyo, walimshtaki ili kuwavutia mitume”[32]

WAGALATIA 1:10-24 NA 2:1-14 : PAULO HAKUPOKEA INJILI YAKE KUTOKA KWA WATU, KAMA KUNDI LA WANA-UHURU LILIVYODAI

Hoja: Katika Wagalatia 1:10-24 na 2:1-14, Paulo anadhihirisha, sio tu kutotegemea kwake mitume huko Yerusalemu, bali pia waamini viongozi wengine wa Kiyahudi ili kukabiliana na madai ya Wana-roho kwamba bado anashikilia chembechembe za Kiyahudi katika ujumbe wake na wala hajaikataa Sheria kwa kiasi cha kutosha, hivyo kukubaliana na matakwa ya Wakristo wa Kiyahudi.

Wagalatia 1:10-24: “Maana, sasa je! ni wanadamu ninaowashawishi, au ni Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo. Kwa maana, ndugu zangu, injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha kuwa sio ya namna ya kibinadamu. Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo. Maana mmesikia habari za mwenendo wangu zamani katika dini ya Kiyahudi, kwamba naliliudhi kanisa la Mungu kupita kiasi, nikaliharibu. Nami naliendelea katika dini ya Kiyahudi kuliko wengi walio hirimu zangu katika kabila yangu, nikajitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zangu. Lakini Mungu, alinitenga tangu tumboni mwa mama yangu, akaniita kwa neema yake, alipoona vema kumdhihirisha Mwanawe ndani yangu, ili niwahubiri Mataifa habari zake; mara sikufanya shauri na watu wenye mwili na damu; wala sikupanda kwenda Yerusalemu kwa hao waliokuwa mitume kabla yangu; bali nalikwenda zangu Arabuni, kisha nikarudi tena Dameski.

Kisha, baada ya miaka mitatu, nalipanda kwenda Yerusalemu ili nionane na Kefa, nikakaa kwake siku kumi na tano. Lakini sikumwona mtume mwingine, ila Yakobo, ndugu yake Bwana. Na hayo ninayowaandikia, angalieni mbele za Mungu, sisemi uongo. Baadaye nalikwenda pande za Shamu na Kilikia. Lakini sikujulikana uso wangu na makanisa ya Uyahudi yaliyokuwa katika Kristo; ila wamesikia tu ya kwamba huyo aliyetuudhi hapo kwanza, sasa anahubiri imani ile aliyoiharibu hapo zamani. Wakamtukuza Mungu kwa ajili yangu”.

Wagalatia 2:1-14: “Kisha, baada ya miaka kumi na nne, nalipanda tena kwenda Yerusalemu pamoja na Barnaba, nikamchukua na Tito pamoja nami. Nami nalikwenda kwa kuwa nalifunuliwa, nikawaeleza injili hiyo niihubiriyo katika Mataifa, lakini kwa faragha kwa hao walio wenye sifa, isiwe labda napiga mbio bure, au nalipiga mbio bure. Lakini Tito aliyekuwa pamoja nami, naye ni Myunani, hakulazimishwa kutahiriwa. Bali kwa ajili ya ndugu za uongo walioingizwa kwa siri ili kuupeleleza uhuru wetu tulio nao katika Kristo Yesu, ili watutie utumwani; ambao hata saa moja hatukujitia chini yao, ili kwamba kweli ya Injili ikae pamoja nanyi. Lakini kwa wale wenye sifa ya kuwa wana cheo; (walivyokuwa vyovyote ni mamoja kwangu; Mungu hapokei uso wa mwanadamu); nasema, hao wenye sifa hawakuniongezea kitu; bali, kinyume cha hayo, walipoona ya kuwa nimekabidhiwa injili ya wasiotahiriwa, kama vile Petro ya waliotahiriwa; (maana yeye aliyemwezesha Petro kuwa mtume wa waliotahiriwa ndiye aliyeniwezesha mimi kwenda kwa Mataifa); tena walipokwisha kuijua ile neema niliyopewa; Yakobo, na Kefa, na Yohana, wenye sifa kuwa ni nguzo, walinipa mimi na Barnaba mkono wa shirika; ili sisi tuende kwa Mataifa, na wao waende kwa watu wa tohara; ila neno moja tu walitutakia, tuwakumbuke maskini; nami neno lilo hilo nalikuwa na bidii kulifanya. Lakini Kefa alipokuja Antiokia, nalishindana naye uso kwa uso, kwa sababu alistahili hukumu. Kwa maana kabla hawajaja watu kadha wa kadha waliotoka kwa Yakobo, alikuwa akila pamoja na watu wa Mataifa; lakini walipokuja wao, akarudi nyuma akajitenga, huku akiwaogopa waliotahiriwa. Na hao Wahayudi wengine wakajigeuza pamoja naye, hata na Barnaba pia akachukuliwa na unafiki wao. Walakini, mimi nilipoona ya kuwa njia yao haiendi sawasawa na ile kweli ya injili, nalimwambia Kefa mbele ya wote, Ikiwa wewe uliye Myahudi wafuata desturi za Mataifa, wala si za Wayahudi, kwa nini unawashurutisha Mataifa kufuata desturi za Wayahudi?”

Wagalatia 1:10-24 haielekezwi tena kwa Wana-uyahudi kama wengine wadhanivyo, bali kwa Wana-roho.[33] Paulo anatamani kuimarisha ukweli kuwa, “Kwa maana, ndugu zangu, injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa sio ya namna ya kibinadamu” (mst.11).

> “Mashtaka ambayo Paulo alikuwa akijitetea mwenyewe kinyume nayo ni lazima yalikuwa kwamba amepokea ujumbe wake kutoka kwa watu, sio kutoka kwa Mungu, kutoka kwa mapokeo, na sio mafunuo.”[34]

Mstari wa kwanza wa waraka huu unasisitiza jambo hili: “Paulo, mtume (sio mtume wa wanadamu, wala kutumwa na mwanadamu, bali na Yesu Kristo, na Mungu Baba…)”

Inashangaza kuwa kwa kweli Paulo hakuelezea kamwe jinsi Mungu alivyoifunua injili kwake. Anajadili tu ukweli kuwa hakuipokea kutoka kwa watu, yaani kutoka kwa watu fulani. (Hajadili kinyume na hoja kwamba kwa ujumla aliipokea kutoka kwa watu).

> “Ushahidi wake unaokanusha hauwezi kuelezewa kama uthibitisho wa tamko yakinifu, bali kama kiashirio kwamba wapinzani wake walidai kwamba amepokea ujumbe wake kutoka kwa watu fulani.”[35]

Mashtaka ya kuwategemea mitume, bila kufikiri yangeweza kuja kutoka kwa Wana-uyahudi, ambao kwao [mitume] walikuwa ni mamlaka. Hata hivyo, dai kuwa mashtaka haya yalikuja kutoka kwa Wana-roho ni lenye kueleweka - walimlaumu Paulo kwa kutozingatia sauti ya Mungu, kama wao walivyodai kuzingatia, bali aliwategemea mitume wa Kiyahudi.[36]

Mistari ya 18 na 21 inathibitisha hitimisho hili.[37] Wakati Paulo ajibupo kuwa alikuwa amekutana na Petro na Yakobo tu, ni lazima hili lilikuwa ni kwa kupinga mashtaka.

> “Yawezekana kiapo hiki kinarejea kwa sehemu kubwa , tena zaidi ya yote, kwenye uhakika kuwa Paulo alikuwa amekutana na Petro na Yakobo tu, na sio mitume wengine; wawili hawa, na ni wawili hawa tu. Ikiwa aapa kwa tamko hili, basi dai dhidi yake ambalo anajitetea mwenyewe kinyume nalo ni lazima likataliwe na kiapo hicho, hususani na sehemu yake inayokanusha,”[38]

Mashtaka dhidi ya Paulo ni lazima yalimhesabia yeye kuhubiri injili isiyo na sheria iliyopokelewa sio kutoka kwa Mungu, bali kutoka kwa mitume fulani. Swali lililozoeleka, “Ni mitume gani waliomaanishwa?” ni muhimu.

> “Hitimisho ni kwamba Paulo hajitetei mwenyewe dhidi ya mashtaka kwamba amepokea ujumbe wake kutoka kwa Petro au Yakobo, bali dhidi ya dai kuwa aliupata kutoka kwa mtume mwingine. Hata hivyo, hakuipokea kabisa kutoka kwa watu, na kwa wakati ule mitume pekee ambao angeweza kupokea ujumbe kutoka kwao walikuwa Petro na Yakobo. Na kwamba angekuwa ameusikia kutoka kwao ni jambo lisilowezekana kabisa.”[39]

Paulo anaendelea na mjadala huo katika sura inayofuata. [40] Hatumii heshima ya mitume kuthibitisha huduma yake ya Ki-Mungu. Hata wakati anapoihakikishia hadhira yake kwamba, “Lakini wale wenye sifa ya kuwa na cheo” ameithibitisha kazi yake, anaongeza, “…walivyokuwa

vyovyote ni mamoja kwangu; Mungu hapokei uso wa mwanadamu…" lakini anapinga alivyohesabiwa kwamba alikubaliana na "ndugu za uongo walioingizwa kwa siri, ambao waliingia kwa siri…" au aliwatii Petro, Yakobo au na mtume mwingine aliyeheshimika (Gal. 2:4-6).

> "Ikiwa twahitimisha kwamba maadui wa Paulo walidai kwamba alilazimisha tohara kutokea Yerusalemu, na kwamba alipaswa kutii, basi hatuna budi kuuliza ni nani aliyeanzisha tetesi? Jibu la kijadi ni Wana-uyahudi. Hata hivyo, sasa, walileta mashtaka kwamba Paulo alijitiisha chini ya mamlaka ya Petro au Yakobo, na heshima ya mafundisho ya tohara"[41]

Wapinzani wa kweli lazima watafutwe miongoni mwa Wana-roho na Wapinga-sheria, waliomlaumu Paulo kwa kukubaliana na matakwa ya tohara.

Hii inathibitishwa katika Wagalatia 2:11-14[42], kwa tamko la Paulo kwamba alishindana na Petro na kumrejeza kwenye ukweli wa injili, hii yaweza kuwa hoja pekee dhidi ya mashtaka ya Wana-roho wasio na sheria, na sio dhidi ya hao Wana-uyahudi.

WAGALATIA 2:15-17 UPENDELEO WA WAYAHUDI UNAPINGA KUNDI LA WASIO-SHERIA

Hoja: Baada ya kudhihirisha kujitegemea kwake kutoka kwa Wana-uyahudi, ambako kulimwezesha kumkemea Petro, mwinjilisti anasisitiza kwa waamini wa Mataifa tofauti baina ya Mataifa na Wayahudi, ambao bado ni watu wa Mungu walioteuliwa. Wengine wote ni wakimbizi kutoka katika ulimwengu wa dhambi.

Wagalatia 2:15-17: “Sisi tulio Wayahudi kwa asili, wala si wakosaji wa Mataifa, hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tuliomwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwanadamu atakayehesabiwa haki. Lakini ikiwa sisi wenyewe, kwa kutafuta kuhesabiwa haki katika Kristo, tulionekana kuwa wenye dhambi, je! Kristo amekuwa mtumishi wa dhambi? Hasha!”

Mimi pamoja na Wilhelm Lütgert na Theodor Zahn[43] tunafikiri kwamba sehemu inayofuata, Wagalatia 2:15-21[44] haipaswi kuwa kwenye kifungu kilichotangulia ambacho ni jibu la Paulo kwa Petro.

> “Maneno haya sio kabiliano, bali utetezi, ambao Paulo asingeuhitaji huko Antiokia, kwa kuwa huko hakupingwa. Bali alimshambulia Petro…”[45]

Hivyo katika sehemu hii Paulo hajitetei mwenyewe dhidi ya Petro, bali kinyume na mashtaka ya Wagalatia. Utetezi wake waanza kwa maneno, “Sisi tulio Wayahudi kwa asili, wala si wakosaji wa Mataifa”,-“sisi” inamaanisha Wakristo wa Kiyahudi. Baada ya kudhihirisha kujitegemea kwake kutoka kwa Wana-uyahudi, ambako kulimsaidia kumpinga hata Petro, anasisitiza tofauti kati ya Wayahudi na Mataifa.

> “Paulo hazungumzi kwa jina la Petro ama kwa jina lake mwenyewe, lakini kama asemavyo waziwazi, katika jina la waamini wote wa Kiyahudi, wale waliokuwa Wayahudi kwa kuzaliwa na wakawa Wakristo. Wamekuwa Wakristo kama Wayahudi, sio kama wale walio wenye dhambi kati ya Mataifa. Hii haimaanishi kwamba wao ni Wayahudi walio bora zaidi ya Mataifa wenye dhambi, bali kama Wayahudi wazaliwa, wao si wenye dhambi kama Mataifa. Hii sio hukumu ya Paulo aliye Myahudi, bali Paulo, mtume. Ingawa msingi wa

> ujumbe wake ni kweli kwamba watu wote hutenda dhambi, hatangazi watu wote kuwa wenye dhambi: bali anatumia maneno haya sio kuelezea sifa waliyonayo watu wote kwa kutenda dhambi, bali kuunda jina la wapagani 'wenye dhambi', wa Mataifa na Waisraeli, ambao hawatambui wala kuishika Sheria"[46]

Paulo anaweza kusisitiza kwamba watu wote ni wenye dhambi (Rum. 3:9, Gal. 3:22), na bado anasema kwamba Wayahudi si wenye dhambi (Gal. 2:5). Anaweza kukubali kwamba aliishi chini ya utawala wa dhambi (Flp. 3:12; Tito 3:3; Rum.7) na bado anadai kuishi bila mawaa mbele ya Sheria (Flp.3:6). Anauona utii wake kwa Sheria kama "mavi" (Flp. 3:8), lakini anamwita Kristo mtimilizaji wa Sheria (Rum.10:4).

Lengo la Paulo hapa ni kuonesha kwa uwazi bila makosa kwamba kuna tofauti kubwa baina ya Mataifa na Wayahudi, na kwamba Wayahudi walioitii Sheria kikamilifu waliishi kwa kulingana na mapenzi ya Mungu, sio kama Mataifa (au Wayahudi) ambao daima hawakutii amri zake.

(Kwa manufaa ya kuelewa, hapa ingekuwa ni jambo lenye msaada kusoma Wagalatia 2:18-21 juu ya Ushika-sheria wa Wana-uyahudi).

WAGALATIA 3:1-29 : AGANO LA AHADI KWA IBRAHIMU NI KUU KULIKO SHERIA, LAKINI HALIFUTI UHALALI WA SHERIA

Hoja: Paulo anakanusha uzushi kwamba utii kwa Sheria waweza kuleta wokovu katika Wagalatia 3, kama ilivyo katika Warumi 4, yenye ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu. Hata katika Agano la Kale ahadi ilitangulia utii na Sheria. Hivyo Sheria ya Musa haiwezi kubatilisha ahadi kwa Ibrahimu. Kwa upande mwingine, ahadi haiwezi kuifanya Sheria isiwe halali, bali inaipa mahali pake halisi katika agano la neema la ki-Mungu pamoja na warithi wake.

Wagalatia 3:1-29: “Enyi Wagalatia msio na akili, ni nani aliyewaloga, ninyi ambao Yesu Kristo aliwekwa wazi mbele ya macho yenu ya kuwa amesulibiwa? Nataka kujifunza neno hili moja kwenu. Je! Mlipokea Roho kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kunakotokana na imani? Je! Mmekuwa wajinga namna hii? Baada ya kuanza kwa Roho, mnataka kukamilishwa sasa katika mwili? Mmepatikana na mateso makubwa namna hii bure. Ikiwa ni bure kweli. Basi, yeye awapaye Roho na kufanya miujiza kati yenu, je! Afanya hayo kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kunakotokana na imani? Kama vile Ibrahimu alivyomwamini Mungu akahesabiwa haki.

Fahamuni basi, ya kuwa wale walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu. Na andiko, kwa vile lilivyoona tangu zamani kwamba Mungu atawahesabia haki Mataifa kwa imani, lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani, kusema, Katika wewe Mataifa yote watabarikiwa. Basi hao walio wa imani hubarikiwa pamoja na Ibrahimu aliyekuwa mwenye imani. Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye. Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; kwa sababu Mwenye haki ataishi kwa imani. Na torati haikuja kwa imani, bali, Ayatendaye hayo ataishi katika hayo. Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti; ili kwamba

baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Kristo Yesu, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.

Ndugu zangu, nanena kwa jinsi ya kibinadamu. Lijapokuwa ni Agano la mwanadamu, hata hivyo likiisha kuthibitika, hakuna mtu alibatilishaye, wala kuliongeza neno. Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, Kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa mzao wako, yaani Kristo. Nisemalo ni hili; agano lililothibitishwa miaka mia nne na thelathini baadaye hailitangui, hata kuibatilisha ile ahadi. Kwa maana urithi ukiwa kwa sheria, hauwi tena kwa ahadi; lakini Mungu alimkarimia Ibrahimu kwa njia ya ahadi. Torati ni nini basi? Iliingizwa kwa sababu ya makosa, hata aje huyo mzao aliyepewa ile ahadi; iliamriwa kwa utumishi wa malaika kwa mkono wa mjumbe. Basi aliye mjumbe si mjumbe wa mmoja; bali Mungu ni mmoja. Basi je! Torati haipatani na ahadi za Mungu? Hasha! Kwa kuwa, kama ingalitolewa sheria iwezayo kuhuisha, yamkini haki ingalipatikana kwa sheria. Lakini andiko limeyafunga yote chini ya nguvu ya dhambi, makusudi hao waaminio wapewe ile ahadi kwa imani ya Yesu Kristo.

Lakini kabla ya kuja kwa ile imani tulikuwa tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa mpaka ije ile imani iliyofunuliwa. Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani. Lakini, iwapo imani imekuja, hatupo tena chini ya kiongozi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo. Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi."

Wagalatia 3:1-4 na 6 inawaelekea Wana-uyahudi na Wana-roho. Wilhelm Lütgert anatambulisha kifungu hiki kwa maneno; "Mchakato wa kimawazo ambao kwa huo Paulo anapambanisha Sheria na Roho unatimiza lengo lake katika 4:6"[47]

Wagalatia 3:1 inazungumza na Wana-uyahudi, wakati kanisa kwa ujumla linatajwa kama "Wagalatia". Lütgert anaueleza mchakato wa mawazo katika Wagalatia 3:1-14 kama ifuatavyo, "Kulikuwa na makundi mawili pinzani katika kanisa, roho huru, ambao waliikataa Sheria; watu washikao sheria, waliomkosa Roho… Paulo alihubiri uhuru wa Roho kutoka kwa Sheria, lakini alipinga mafikara ya kutokuelewana ya

makundi hayo mawili. Msimamo wake juu ya Roho na Sheria uliwapinga wote wana-sheria na wana-roho."[48]

Acha tufikiri wazo la Agano la Kale katika Wagalatia 3. Mungu kwa sababu ya ahadi yake na neema yake, amefanya mkataba na Mwanadamu. Mkataba huu unaonesha majukumu halisi, ambayo yanafasiliwa na Sheria. Kwa kutegemea uelewa wao wa Wagalatia 3 na Waebrania 9, Wakristo wengi wanaothibitisha umuhimu wa Agano katika Agano la Kale, wanatilia mashaka jukumu lake katika lile Jipya, ambalo, hata hivyo, ni Agano Jipya, kama injili yake inavyoitwa katika Agano la Kale na katika lile Jipya.

Kwa kulingana na Wagalatia 3:17, Ahadi na agano la neema la Mungu viliitangulia Sheria; "…Agano lililothibitishwa kwanza na Mungu, Sheria iliyotokea miaka mia nne na thelathini baadaye hailitangui, hata kuibatilisha ile ahadi". Wengi hulitafsiri tamko hili kumaanisha kwamba Sheria imetanguliwa na kuwa kitu bure. Hata hivyo, Paulo hasemi hivyo, bali anathibitisha uhalali wa Ahadi, na hivyo wa Agano. Wagalatia 3:21 inalidhihirisha hili kwa uwazi, "Basi je! Torati haipatani na ahadi za Mungu? Hasha! Kwa kuwa kama ingelitolewa sheria iwezayo kuhuisha, yamkini haki ingalipatikana kwa sheria." Sheria haiwezi "kuhuisha" bali ilitolewa "kwa sababu ya makosa" (Gal.3:19).

Kwa kudhamiria nimechagaua neno "agano" badala ya "patano". Neno la Kigriki, 'diatheke' linatumiwa daima katika Septuaginti (Maandiko Matakatifu kwa Kigriki) mahala pa neno la Kiebrania 'berith'-'agano'. Dhamira ya Paulo katika Wagalatia 3:15-18 ni ukweli kuwa agano haliwezi kutanguliwa au kufutwa. Wazo kuwa Mungu alifanya patano kwa uwezekano kuwa aweza kufa, si la kibiblia kabisa na ni upuuzi. Tamko, "lijapokuwa ni agano la mwanadamu, hata hivyo likiisha kuthibitika, hakuna mtu alibatilishaye, wala kuliongeza neno" kwa urahisi linasisitiza kwamba agano la ki-Mungu haliwezi kutanguliwa au kufutwa. Wakitafsiri mstari wa 17 kuelezea agano, Daniel C. Arichea na Eugene A. Nida wanapendekeza:

> "Je! neno hili linamaanisha 'dhamiri' ('patano') na uhusisha mtu mmoja tu…? Au neno hili linapata wazo lake kutoka katika wazo la Kiebrania la 'agano' ('mkataba'), na kwa namna ile ile uhusisha washiriki wawili…? Matumizi ya kibiblia ya neno na muktadha mzima unakubaliana na mbadala wa pili."[49]

Kifungu kinaelezea agano lililofanywa na Mungu pekee, lakini likiwa na majukumu pande zote mbili. Hivyo tu ndivyo Paulo anaweza

kulinganisha Agano na Ahadi, na kuongea juu ya “agano la ahadi” mahali popote (Efe. 2:12). Paulo anadhihirisha, mrithi wa kweli ni Kristo (Kol. 1:12-18), ambaye katika yeye ahadi zote zinatimizwa. “Maana Mwana wa Mungu, Kristo Yesu… hakuwa Ndiyo na Siyo; bali katika yeye ni Ndiyo” (2 Kor. 1:19-20). Basi hii inamaanisha kwamba, Paulo anatafsiri Agano la Kale kwa mpango wa kufuata miaka, jambo lifanyalo wazo kuwa Kristo ni mpinzani wa moja kwa moja wa ufunuo wa Agano la Kale kuwa kichekesho.[50]

‘Diatheke’ yapaswa kutafsiriwa kama ‘agano’ katika Waebrania 9:16-17[51] “Kwa maana mahali palipo na agano, mtu aliyeliwekea muhuri agano lile lazima afe. Kwa kuwa agano lina nguvu baada ya kifo, kwa sababu haliwezi kuwa halali, ikiwa aliyelifanya agano bado yungali anaishi.”(Tafsiri ya mwandishi). Hii haimaanishi kwamba Kristo alipaswa kufa, kwa sababu patano lingeweza tu kufanya kazi baada ya kifo chake, bali kwa sababu, kama agano, lingeweza kufanywa imara kwa damu tu, kwa kupoteza maisha, yaani kama ilivyokuwa katika Agano la Kale mnyama alipotolewa dhabihu kuthibitisha agano (Mwa. 15; Law. 1). Kama kilivyo kifo cha mtu hakilifanyi patano kuwa halali tu, bali pia kinalifanya agano liwe katika vitendo, ili kwamba mrithi aweze sasa kurithi; ndivyo ilivyo kwa kifo cha Kristo kilithibitisha Agano la Mungu badala ya kulitangua.

Katika Wagalati 3:6-29, Paulo anadhihirisha kwamba Ahadi kwa Ibrahimu, ambayo kwayo Wayahudi hurejea daima, ilitangulia utoaji wa Sheria katika mlima Sinai, na huo ni uthibitisho usiokanushika kwamba kuhesabiwa haki hutegemea Ahadi na Imani, na sio utunzaji wa Sheria. Sababu muhimu iliyomfanya Ibrahimu “Baba wa Mataifa mengi”, sio suala juu ya urithi wa kibaolojia na wala sio uhalali wa kisheria wa utii wa Sheria, bali ni tumaini lake lisilo mpaka katika ahadi ya Mungu (Waeb.11:8-9).

Swali, “Akina nani ni watoto wa Ibrahmu?” linajadiliwa sio tu katika Wagalatia 3, bali pia katika Warumi 4[52] na katika maandiko mengine mengi. Kwa upande mwingine, Wayahudi wote wanatajwa kama watoto wa Ibrahamu kwa mujibu wa mababu zao (Mdo. 13:26), lakini Wayahudi wasioamini wanakosa dai hilo kwa sababu ni imani pekee iwezayo kumfanya mtu mtoto wa Ibrahimu. Yohana 8:37-40 ni mfano halisi wa pande hizi mbili, “Najua kuwa ninyi ni uzao wa Ibrahimu…” wakati mwingine, Yesu anasema kwamba Mungu aweza kumwinulia Ibrahimu watoto kutoka kwenye mawe ili kuchukua sehemu ya Mafarisayo na

Masadukayo (Mat. 3:9, Luka 3:8), hili halirejei kwa dhabihu ya Isaka tu, bali pia Mataifa kufanywa wana wa Ibrahimu kwa sababu ya imani yao. Mataifa wataketi pamoja na Ibrahimu katika ufalme wa mbinguni, kwa mujibu wa Yesu; jambo litakalowafanya Mafarisayo, ambao watatupwa katika giza la nje, kusaga meno yao (Mat.8:11-12; Luka 13:28). Wayahudi mara nyingi wanaamini kuwa wanaitwa 'watoto wa kike na wa kiume wa Ibrahimu' (Luka 13:16; 19:6). Tukirejea kwa Wayahudi na Mataifa, Paulo anasema, "wale walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu" (Gal. 3:7, linganisha na mistari ya 8-9 na 14-18), kwa kuwa "Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi" (Gal. 3:29).

WAGALATIA 3:8-14 : JE, SHERIA INAJIPINGA YENYEWE?

Wagalatia 3:8-14: “Na andiko, kwa vile lilivyoona tangu zamani kwamba Mungu atawahesabia haki Mataifa kwa imani, lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani, kusema, Katika wewe Mataifa yote watabarikiwa. Basi hao walio wa imani hubarikiwa pamoja na Ibrahimu aliyekuwa mwenye imani. Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye. Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; kwa sababu Mwenye haki ataishi kwa imani. Na torati haikuja kwa imani, bali, Ayatendaye hayo ataishi katika hayo. Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti; ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Kristo Yesu, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.”

Kwa mujibu wa Ragnar Bring[53], sura ya tatu ya Wagalatia, hususani mstari wa 12, unadhihirisha uwiano mkubwa na Warumi 10:4-5. Kwa sababu hii, basi tuchunguze Warumi 10:4-5.

Katika Warumi 10:4-8, Paulo anasema, “Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria, ili kila aaminiye ahesabiwe haki. Kwa maana Musa aliandika juu ya haki itokayo kwa sheria, ya kuwa, Mtu afanyaye hiyo ataishi kwa hiyo. Bali ile haki ipatikanayo kwa imani yanena hivi, Usiseme moyoni mwako, Ni nani atakayepanda kwenda mbinguni? (Yaani, ni kumletea Kristo chini), au, ni nani atakayeshuka kwenda kuzimuni? (Yaani ni kumleta Kristo juu, kutoka kwa wafu.) Lakini yanenaje? Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako; yaani, ni lile neno tulihubirilo.”

Kwa nini Waisraeli katika kumkataa Kristo, hawakujali haki na Sheria (Rum.10:2-3)? Walimkataa Kristo, aliye mwisho wa sheria. Neno la Kigriki ‘telos’ lina maana nyingi, na linapaswa kutafsiriwa kama ‘mwisho’ au ‘kusudi’. Tafsiri hutegemea imani ya mtafsiri juu ya Sheria ya Musa. Kwa maoni yangu, tafsiri, “Kristo ni utimilifu (au lengo) la sheria” inaakisi vema maelezo ya Paulo juu ya Sheria katika Warumi (kwa mfano, 3:20, 31; au 7:7, 12-16, 22-24; 8:3-4, 13:8-10).[54] Sheria yote inatafuta lengo lake, maana yake, ukamilifu wake na utimilifu wake katika Kristo.

“Kristo ni lengo, nia, kusudi, maana halisi na kiini cha sheria - mbali na yeye, haiwezi kabisa kueleweka vema.”[55]

Kifungu kinapendekeza tafsiri ya, “ ‘lengo’ kwa nguvu sana. Hiyo pekee kwa utoshelevu inatoa taswira ya mbio.”[56]

Kwa hiyo sentensi hii inalingana kimakusudi na Warumi 13:10 “Pendo ndilo utimilifu wa sheria” na tamko la Yesu katika Mat. 5:17, ingawa mifano hii miwili inatumia neno la wazi zaidi kwa “utimilifu”. Kutafsiri Warumi 10:4 kumaanisha kuwa Kristo ni mwisho wa Sheria; kwamba aliifanya Sheria isiwe halali, ili kwamba isiweze kutiiwa, kungepingana na kila kitu Paulo anachopaswa kusema juu ya maisha ya kimaadili ya mwamini (Kwa mfano, Rum. 8:3-4, au 13:8-10).

Wengine huielewa Warumi 10:5 kuwa inaeleza wokovu wa Agano la Kale kwa matendo (“Mtu afanyaye hivyo ataishi kwa hiyo”), wakati mstari wa 6 na kuendelea huelezea wokovu wa Agano Jipya kwa imani. Tafsiri hii haijali ukweli kwamba katika hali zote mbili, Paulo ananukuu kutoka katika Agano la Kale! Je, Paulo anampinga Musa kwa kumtumia Musa yule yule (Law. 18:5=Rum. 10:5; Kum. 30:12-14=Rum. 10:6-8)? Je, anakusudia kutangua Mambo ya Walawi 18:5 kwa kunukuu Isaya 28:16 (=Rum. 10:11) au Yoeli 2:32 (=Rum. 10:13)?

Muktadha wa Warumi 9:30-32 unaifanya tafsiri hii kuwa isiyowezekana. Felix Fluckiger, katika insha yake bora kabisa juu ya Warumi 10:4, asema:

“Tamko kwamba Wayahudi waliokuwa wanaifuata Sheria ya haki, hawakuipata, linafanya (tamko lenyewe) kuwa lisilowezekana kwa kuufanya wokovu wa Kiyahudi kwa matendo njia sahihi ya kufikiri haki kwa kulingana na matakwa ya Torati”[5]

Hali ya kuendeleza mjadala wa tamko haimpingi Musa-hili laweza kuonekana katika ukweli kwamba Paulo ananukuu Sheria ya Musa mara tatu (Kum. 30:12-14). Yeye anawashambulia Wayahudi, ambao awali waliipinga, mtazamo wa kimakosa wa Sheria unapingwa na Sheria yenyewe.”[58]

Basi ni kwa nini Paulo anamnukuu Musa katika Warumi 10:5? Felix Fluckiger anaeleza:

> Musa anadai kwamba haki inayotakiwa na Sheria ni lazima itekelezwe ikiwa mtu anataka kuishi, lakini takwa hilo halihitaji kutimizwa kwa mafanikio ya mtu mwenye uwezo usio wa kawaida, bali kwa neno moyoni na kinywani, ambalo, kwa mujibu wa Warumi 10:10, ni

> imani…Maisha yaliyoahidiwa katika 10:5 yanakuwa kwa mtu anayeamini na kukiri. Utii wa imani unaonekana kuwa timizo halisi la Sheria."[59]

Ikieleweka vema, Paulo analinganisha Sheria ya Agano la Kale na Kristo, umuhimu na lengo lake, na imani katika yeye.[60] Paulo analifanya hili bayana katika Warumi 10:7 kwa kumweka Yeye mahali pa Sheria katika nukuu za Kumbukumbu la Torati 30:12-14.[61]

Walter C. Kaiser, anayeshiriki mtazamo wa Fluckiger, anaonesha[62] kwamba 'maisha' yaliyotolewa na Sheria si maisha ya milele, bali furaha na utimilifu katika dunia.[63] Sheria huahidi maisha timilifu na salama duniani, lakini sio maisha ya milele au wokovu. Kaiser anashikilia hili kuwa ukweli wa kipekee anaporejea katika Mambo ya Walawi 18:5, ambayo Paulo anainukuu katika Warumi 10:5, "Mtu afanyaye hiyo ataishi kwa hiyo."

Tugeukie tena kwa Wagalatia 3. Kama ilivyo katika Warumi 10, Paulo anajenga msingi wake wa upinzani kwa Ushika-sheria wa Agano la Kale na Sheria yenyewe. Imani si kitu kigeni kwa Sheria, bali ina mizizi katika hiyo. " Na andiko kwa vile lilivyoona tangu zamani kwamba Mungu atawahesabia haki Mataifa kwa imani…"(Gal. 3:8).

Paulo analinganisha laana ya Agano la Kale juu ya kuhesabiwa haki kwa Sheria na baraka ya Agano la Kale juu ya imani.. "Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, *(au wale wanaotegemea matendo ya sheria),* wako chini ya laana; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye. Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; kwa sababu Mwenye haki ataishi kwa hiyo" (Gal.3:10-11).

"Maelezo 'wale wanaotegemea katika kuitii sheria' yanajumuisha mambo yaliyoachwa ya kimaana (kisemantiki), kwa kuwa lengo la utegemezi limekwisha ondolewa; kwa maneno mengine, hawa ni watu ambao wanategemea katika kuitii Sheria ili waweze kuwekwa kuwa sawa na Mungu…Kwa hiyo, yaweza kuwa muhimu kutafsiri kishazi hiki kama 'wale ambao wanadhani watakubaliwa na Mungu kwa sababu wanatii kile ambacho sheria zinasema."[65]

Katika kuonya dhidi ya "kazi (au matendo) ya sheria",[66] (Gal. 2:16, 3:2, 10; Rum. 3:20, 28), Paulo haonyi dhidi ya kufanya kile ambacho Sheria inaeleza. Anasifu kazi ya Kikristo, ambayo kwa ujumla anaisifu kwa maelezo yakinifu, kama vile 'kazi za imani' (1The.1:3, 2The.1:11).

Anatumia maelezo ‘Kazi za Sheria’ kuyafanya yale yafanywayo ili yalipwe kwa wokovu. Anatofautisha kati ya kazi zifanywazo kwa haki binafsi, ambazo zinapaswa kukataliwa; na kazi za imani ambazo anazisifu (kwa mfano, Tito 3:1, 5, 8; Efe. 2:8-10). Kwa hiyo, kuna tofauti kati ya utii (wa kimakosa) ili kujipatia wokovu, na kwa upande mwingine utii unaoibuka kama zao la imani.[67]

Ingeweza kuwa makosa kabisa kutafsiri Wagalatia 3:10-11 kama laana juu ya wote, ambao kwa sababu fulani, wanataka kushika amri za Mungu, kama afanyavyo Theodore H. Epp, anayesema, “watu wanalaaniwa wakati wanapojaribu kutunza Sheria.”[68] Ragnar Bring anaandika, “Sio Sheria yenyewe ambayo, kwa mujibu wa Paulo, iko katika nguvu za dunia hii, bali ushika-sheria.”[69]

Martin Luther, ambaye tafsiri yake ya Waraka kwa Wagalatia mara nyingi inatofautiana na yetu,[70] alipata mgawanyo sawa katika mahubiri juu ya Wagalatia 3:23-24, “Kwa kuwa Kristo ametuweka huru kutoka katika laana ya Sheria, sio kuacha kuitii”[71]

Hivyo, “Kristo ametukomboa sisi kutoka katika laana ya sheria, akiwa ni laana kwa ajili yetu.” Paulo anatetea kanuni hii kwa msingi wa Sheria yenyewe: “Amelaaniwa kila aangikwaye juu ya mti” (Gal. 3:13, tazama Kum. 21:23), ili kwamba “baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani” (Gal. 3:14). Hapa tena, Paulo halinganishi Agano la Kale lenye Sheria na Agano Jipya lenye Ahadi na Injili. Bali, anaichukua Ahadi kutoka Agano la Kale, kutoka katika vitabu vitano vya Musa, hii ni kumaanisha kutoka katika Sheria yenyewe.

WAGALATIA 3:13-14 : MATAIFA PIA WANAKABILIWA NA HUKUMU CHINI YA SHERIA

Hoja: Kama ilivyo katika Wagalatia 4:1-18, Wagalatia 3:13-14 inadokeza kwamba Kristo hakuwakomboa Wakristo wa Kiyahudi tu kutoka katika laana ya Sheria, bali pia waamini wa Mataifa. Sheria inawafunga wanadamu wote, kama ulivyo uhuru kutoka katika hukumu na laana yake kwa kifo cha Yesu Kristo, (Kifo cha Yesu) ni chenye kufanya kazi na kuleta matokeo kwa Wayahudi na Mataifa vilevile.

Wagalatia 3:13-14: "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti; ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani."

Kwa mujibu wa Wagalatia 3:13-14, Mataifa wamekwishawekwa huru kutoka kwa Sheria, kama ilivyo kwa Wayahudi.

> "Utambuzi wa makusudi ya jumla ya Mungu kuwaokoa Wayahudi na Mataifa kwa kifo cha dhabihu ya Kristo, unamsukuma Paulo kutumia kinyume nyume ujumla uleule wa makusudi ya kuokoa ya ki-Mungu. Tendo la kwanza la huduma ya wokovu, Utoaji-sheria, ni halali kwa huduma ya wokovu ya jumla kwa Mataifa na vilevile kwa Wayahudi. Kwa muda wote sheria ilipokuwepo, hadi ujio wa Kristo, kanuni yake ilikuwa halali kwa wote (Wagalatia3:10-12)"[72]

Ragna Bring anaandika, "Wagalatia, kwa wingi, waamini wa Mataifa, wanajumuishwa katika kundi la wale ambao wako chini ya Sheria."[73] Na Lütgert asema:

> "Kwa hiyo, Sheria sio dini ya Wana wa Israeli tu, bali ni kanuni kwa historia yote. Ulimwengu unaongozwa na kuamriwa na yenyewe. Huu ndio umuhimu wake katika injili ya Paulo. Sio Israeli tu, bali mataifa yote yako chini ya Sheria na yanahukumiwa kwa yenyewe. Hivyo, ingawa hawakushiriki katika dini ya Israeli, wokovu humaanisha ukombozi pia kwa Mataifa kutoka kwa sheria, kanuni hususani inayojadiliwa katika Waraka kwa Wagalatia."[74]

Wagalatia 3:22-28 inadhihirisha wazi kwamba, wakati Sheria ilipowatenga wanadamu katika Wayahudi na Mataifa, Ahadi iliyotimizwa ilifanya kinyume chake.[75] Kumbuka kuwa mchakato mzima wa

kimawazo wa Paulo waweza tu kueleweka wakati mtu aonapo ukweli kwamba, anaamini Mataifa kuwa, kama ambavyo wamekuwa daima, watii kwa Sheria.[76] (Tutarudi katika mjadala huu katika sura ya Wagalatia 4:1-18).

WAGALATIA 3:19-21 : MALAIKA NA SHERIA

Hoja: Kristo ni mjumbe wa kweli wa Sheria. Sifa yake ya uungu haidunishwi na ukweli kwamba malaika ndio walioiwasilisha.

Wagalatia 3:19-21: “Torati ni nini basi? Iliingizwa kwa sababu ya makosa, hata aje huyo mzao aliyepewa ile ahadi; iliamriwa kwa utumishi wa malaika kwa mkono wa mjumbe. Basi aliye mjumbe si mjumbe wa mmoja; bali Mungu ni mmoja. Basi je! Torati haipatani na ahadi za Mungu? Hasha! Kwa kuwa, kama ingalitolewa sheria iwezayo kuhuisha, yakini haki ingalipatikana kwa sheria.”

Katika Wagalatia 3:19 Paulo anajadili umuhimu wa Sheria. Swali hili laweza tu kuwa lililoanzishwa na Wakristo wa Mataifa.[77]

Kwa kusisitiza katika mstari wa 20, kwamba mjumbe “mmoja” anatenda kwa ajili ya kundi, Paulo anaeleza kuwa sio wazao wa Ibrahimu - watu wa Israeli kwa ujumla wao- ndio wajumbe, bali ni Kristo tu, Mzao kwa umoja wake, anayeweza kufaa kwa jukumu hili.[78] Israeli haiwezi kuwa mjumbe, kwa sababu lenyewe linamhitaji mtu mmoja.

Rejea kwa malaika waliowasilisha Sheria kwa mwanadamu (Gal. 3:19), hii haipingani na asili ya ki-Mungu ya Torati[79]. Katika Matendo 7:53, anauchukua uthibitisho wake wa asili yake ya ki-Mungu kwa kurejea katika ushiriki wa malaika.[80] Ufunuo wa Sheria kwa njia ya malaika hauwezi kumaanisha kuwa Sheria sio ya ki-Mungu na hivyo isichukuliwe kwa umakini, bali kwa injili iliyofunuliwa moja kwa moja katika Mwana wa Mungu pasipo uingiliaji wa malaika, ni yenye utukufu zaidi (Tazama 2Kor.3:10-11).[81] Ukweli kuwa malaika waliiwasilisha Sheria ya Musa hauondoi ushiriki wa Yesu katika utoaji wa Sheria juu ya mlima Sinai. Ni jambo lenye umuhimu mkubwa kwa maadili, kuwa Agano Jipya huona kuwa Yesu mwenyewe ndiye aliyempa Musa Sheria. Kama ushahidi wa Agano la Kale, Herman Witsius ananukuu Zaburi 68:18. Waefeso 4:8 inaonesha kuwa kifungu hiki kinaakisi kupaa kwa Kristo kuelekea Mbinguni. Hata hivyo, Mtu wa ki-mbingu anayetajwa katika mstari wa 18, ni sawa na yule yule ambaye aliwaongoza Israeli katika jangwa, Mlima wa Sinai (Zab.68:18), ambaye alimfunulia Sheria Musa mahali pale.[82] Kwa hali zote mbili, Zaburi hurejea kwa Yesu Kristo. Witsius anarejea zaidi kwa mahubiri ya Stefano ambayo yanamlinganisha Malaika wa BWANA ambaye

aliongea na Musa katika kichaka kiwakacho moto (Mdo.7:35) na ambaye, kwa kulingana na Mababa wa Kanisa na Wana-Matengenezo, analinganishwa na Yesu[83], ambaye pia alikuwa Malaika aliyewaokoa Israeli kutoka utumwani Misri, aliyewaongoza kupita katika Bahari ya Shamu na katika jangwa na aliyempa Musa Sheria (Mdo.7:38).[84]

WAGALATIA 3:24 : SHERIA KAMA KIONGOZI

Hoja: Thamani ya sheria iko katika jukumu la kuelimisha na kumwandaa mtu kwa ajili ya Kristo. Hivyo basi haina maana pasipo Yeye. Uhuru wetu katika Kristo unabadilisha mahusiano yetu kwa Sheria, lakini sio uhalali wa yale yaliyomo.

Wagalatia 3:24-26: “Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani. Lakini, iwapo imani imekuja, hatupo tena chini ya kiongozi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu.”

Kipekee, John Calvin amesisitiza kuwa Agano la Kale linatuelimisha kwa maandalizi ya Agano Jipya.[85] Herman Witsius, akirejea kwa Wagalatia 4:2 analiita Agano la Kale “mausia ya utoto” kwa kuwa, “kwa ujumla lilikuwa la kufunza na lililofaa kwa watoto”.[86] Kwa maoni ya Witsius amri, “Msishike, msionje, msiguse” (Kol. 2:21) ambayo kwayo Paulo anaelezea sheria za maadhimisho za Agano la Kale, sawa kabisa na sheria wanazopewa watoto. Wagalatia huelezea mtazamo wa ukuaji ambao kwao watu wa Mungu huanza na njia ndogo katika historia ya familia kutoka kwa Adamu mpaka kwa Abrahamu, kisha hukua kupitia maagano mbalimbali katika Kristo na mwili wake duniani pote. “Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani. Lakini, iwapo imani imekuja, hatupo tena chini ya kiongozi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu” (Gal. 3:24-26).

Wengi hutafsiri kifungu hiki kumaanisha kuwa kiongozi si muhimu tena, kwani tu wana wa Mungu. Kwa kweli kifungu kinasema kwamba 1. Sheria yote inaelekezwa kwa Kristo na kwa kuhesabiwa haki kwa imani (“kwa Kristo, ili…”) na kwamba 2. kipindi cha elimu chini ya utumwa kimekwisha kwa mahusiano ya moja kwa moja ya mtoto na Baba wa Mbinguni. Hii haiathiri viwango, bali nafasi tu. Upinzani hauko kati ya uhalali wa Sheria na kumalizwa kwake, bali kama Herman N. Ridderbos anavyoandika, kati ya “maisha machanga ya utumwa chini ya kiongozi” na “maisha ya uana pamoja na mapendeleo na haki zake.”[87]

Hata katika Agano la Kale, Sheria ilihudumia lengo la kielimu - Neno la Kiebrania kwa Sheria, ‘torah’ [Kiswahili: ‘torati’], kihalisia humaanisha

“maelekezo au mafundisho”. Mungu anatufundisha wanadamu kwa Neno lake na kwa Sheria yake. “Hivyo torati imekuwa kiongozi (Kigriki-‘paidogogos’) kutuleta kwa Kristo.” Utendaji huu unaonekana kipekee katika makuzi ya watoto. Ikiwa Paulo anaijali Sheria kuwa mwalimu na anaihusisha na Kristo, basi anasisitiza umuhimu wa jina lake, ‘torati’, maana ambayo daima imekuwa katika Agano la Kale.

Kwa wenye dhambi na wasioamini, Sheria hubaki kuwa “kiongozi”, kwa kuwa Sheria huongoza kwenye uhakikishi wa habari ya dhambi, ambao ni lazima utangulie ukombozi kutoka katika laana ya Sheria. Roho Mtakatifu humwonesha mtu dhambi zake kwa kupitia Sheria. “Naye [=Roho Mtakatifu] akiisha kuja, huyo atauhakikishia ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu”(Yohana 16:8, linganisha na mst.16).

Theolojia ya Matengenezo hutofautisha majukumu matatu ya sheria ya maadili ya kibiblia:[88]

1. Jukumu la Kisiasa (Kilatini:- ‘usus politicus’)[89] humaanisha kuwa Sheria ni ‘njia lazimishi za nje au za wazi’ za kupima dhambi hatari’[90] na makosa hatari.

2. Jukumu la Elimu au Uhakikishi (Kilatini:- ‘usus pedagogicus’ au ‘usus elenchticus’[91]) humaanisha kuwa Sheria humhakikishia dhambi mwenye dhambi, humhukumu na humwelimisha (kama kiongozi, Kigriki-‘paidogogos’) kumwelekea Kristo. Jukumu hili ni muhimu kwa kazi ya uinjilisti.

3. Jukumu la Uongozi (‘usus didacticus’) humaanisha kuwa Sheria humpa mwamini aliyezaliwa mara ya pili sheria za kuishi kwazo. Anashika sheria kwa nguvu za Roho Mtakatifu, sio ili apate wokovu.

Muhimu kwa kiini cha somo la Wagalatia ni ukweli kwamba kazi ya pili ya Sheria bado ni muhimu leo katika uinjilisti na nidhamu ya kanisa, na haitangui kazi ya tatu.

WAGALATIA 4:1-20 : MATAIFA PIA WANAWEKWA HURU KUTOKA KATIKA KAWAIDA ZA KWANZA ZA DUNIA

Hoja: Kwa mujibu wa Maandiko, sio tu Wayahudi waliokwishakombolewa, bali pia Mataifa ambao walikuwa watumwa wa kawaida za kwanza za kidunia.

Wagalatia 4:1-20: “Lakini nasema ya kuwa mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote; bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati uliokwisha kuamriwa na baba. Kadhalika na sisi, tulipokuwa watoto, tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia. Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye Aba, yaani, Baba. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.

Lakini wakati ule, kwa kuwa hamkumjua Mungu, mliwatumikia wao ambao kwa asili si miungu. Bali sasa mkiisha kumjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu, kwa nini kuyarejea tena mafundisho ya kwanza yaliyo manyonge, yenye upungufu, ambayo mnataka kuyatumikia tena? Mnashika siku, na miezi, na nyakati, na miaka. Nawachelea, isiwe labda nimejitaabisha bure kwa ajili yenu.

Ndugu zangu, nawasihi, iweni kama mimi, maana mimi ni kama ninyi. Hamkunidhulumu kwa lolote. Lakini mwajua ya kuwa naliwahubiri Injili mara ya kwanza kwa sababu ya udhaifu wa mwili; na jaribu lililowapata katika mwili wangu hamkulidharau wala kulikataa, bali mlinipokea kama malaika wa Mungu, kama Kristo Yesu. Ku wapi, basi, kule kujiita heri? Maana nawashuhudu kwamba, kama ingaliwezekana, mngeling’oa macho yenu, mkanipa mimi. Je, nimekuwa adui wenu kwa sababu nawaambia yaliyo kweli? Hawa wana shauku nanyi, lakini si kwa njia nzuri, bali wanataka kuwafungia nje, ili kwamba ninyi mwaonee wao shauku. Navyo ni vizuri kuonewa shauku katika neno jema siku zote, wala si wakati nikiwapo mimi pamoja nanyi tu. Vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu; laiti

ningekuwapo pamoja nanyi sasa, na kuigeuza sauti yangu! Maana naona shaka kwa ajili yenu".

Kumekwisha kuwepo majadiliano mengi juu ya tamko, "Kadhalika na sisi, tulipokuwa watoto, tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia". Wagalatia 4:8-11 yaendelea, "Lakini wakati ule, kwa kuwa hamkumjua Mungu, mliwatumikia wao ambao kwa asili si miungu. Bali sasa mkiisha kumjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu, kwa nini kuyarejea tena mafundisho ya kwanza yaliyo manyonge, yenye upungufu, ambayo mnataka kuyatumikia tena? Mnashika siku, na miezi, na nyakati, na miaka. Nawachelea, isiwe labda nimejitaabisha bure kwa ajili yenu".

"Kawaida za kwanza za dunia" imekwisha fasiliwa kuwa ni malaika au mapepo, na kawaida za kwanza kuwa ama sherehe za kipagani au maadhimisho ya sheria za Agano la Kale. Ulinganishaji wowote wa malaika na kawaida za kwanza za dunia ni lazima ukataliwe.[92] Kulinganisha kawaida za kwanza na sheria za Kiyahudi ni vigumu, kwa kuwa muktadha unaonekana kuzungumza na Mataifa. Mstari wa nane unaonya wazi dhidi ya kurudia dini ya kipagani, kwa kuwa huzungumzia waabudu sanamu wa zamani. Je, yawezekana kuirudia sheria ya Kiyahudi kwa kuabudu sanamu? Lütgert anashikilia sawasawa kuwa 'kawaida za kwanza za dunia' ni desturi za kujikana za kipagani. [93]

"Ikiwa ushiriki katika sherehe za kipagani ulipata njia yake kuingia katika Kanisa la Galatia kama ilivyokuwa huko Korintho" [94] tamko la Paulo, "Nawachelea, isiwe labda nimejitaabisha bure kwa ajili yenu" ni lenye kueleweka.

Ikiwa, kama Lütgert anavyopendekeza, "kawaida za kwanza za dunia" ni sherehe za kipagani na sheria za kujikana, na sio sheria za Agano la Kale,[95] basi kifungu ni lazima kinazungumza na Mataifa waliopinga Sheria na sio Wayahudi washika-sheria.

Ragnar Bring vilevile analinganisha Wagalatia 4:10 na Wakolosai 2:14, kifungu ambacho anakihusisha na sheria za maadhimisho ya Agano la Kale na pia sherehe za kuabudu sanamu.

> "Anasisitiza sifa ya mitazamo ya uzushi wa Wagalatia na Dini ya Kiyahudi."[96]

Kwa kweli kuna mifanano. Maadhimisho ya kisheria hurekebisha tabia zenye kuelekea kwenye kawaida za kwanza za dunia, vitu vya nje na matendo, kwa mfano, kile ambacho mtu hawezi kugusa, kula au

kufanya, katika nyakati fulani. Wakati Wayahudi wamepokea sheria za ki-Mungu kwa hali ya utoto wa mwanadamu, Mataifa hawakuwa na chochote. Sasa hayo mafunzo ya utoto yamefikia mwisho, Wayahudi na Mataifa wako sawasawa katika kukombolewa kutoka katika kawaida za kwanza za dunia. “Sheria ni elimu ya awali ya binadamu”[97]. Mahusiano yasiyochanganya ambayo Wakristo wa Agano Jipya waweza kuwa nayo kwa Asili na kwa vitu vya nje, ni kwa sababu ya mafunzo ya utotoni ambayo Mungu amewapa katika Agano la Kale na kwa kifo cha kidhabihu cha Kristo msalabani, ambacho kilifikisha mwisho utoto na kuwafanya wenye kustahili kupokea urithi wao. George Huntemann amesisitiza hili barabara na kwa nguvu:

> Chini ya utawala wa Kristo - na ni hapa tu-Uumbaji uko huru. Sheria za usafi za Agano la Kale hutukumbusha daima na pasipo ukatili kwamba (uumbaji) umekwisha kukombolewa, yaani wamiliki wasio halali wa Uumbaji wamekwisha shindwa vitani, lakini bado hawajaharibiwa.”[98]

Wagalatia 4:12-20 ni lazima ijadiliwe katika muktadha huu, hususani mtajo wa “udhaifu” wa Paulo katika mstari wa 13 na 15, [99] ambao kwa kawaida unaaminika kurejea tatizo la jicho, lakini ambalo laweza kupata umuhimu mwingine tofauti katika muktadha wa mgongano na Wana-roho.

> “Sehemu nzima haihitaji kurejea kwa ugonjwa, bali yaweza kuhusika na udhaifu wa mwili kwa kupingana na nguvu za Sheria…Mistari inapaswa kueleweka kama alivyofanya Calvin… Paulo aliishi katika Galatia kama alivyofanya katika Korintho, bila kufanya mvuto mkubwa wa nje; hakuonekana au kufanya kama mbebaji wa ufunuo wa ki-Mungu.”[100]

John Calvin anaandika,

“Kwa ‘udhaifu wa mwili’ Paulo alimaanisha kitu chochote kilichomfanya aonekane dhaifu na duni, ‘mwili’ huelezea mwonekano wa nje, hivyo basi, ‘udhaifu wa mwili’ hudokeza mwonekano usiovutia…”[101]

Swali katika mstari wa 21 (“Niambieni, ninyi mnaotaka kuwa chini ya sheria, je! Hamwisikii sheria?”) linakuwa lenye kueleweka ikiwa Wagalatia 4:8-20 inajishughulisha na wakereketwa wa Mataifa.[102] Kisha Paulo anarudi kwenye tatizo la Wayahudi. Anaelezea tofauti baina ya wokovu kwa matendo na wokovu kwa neema na Ahadi; kwa kutumia mfano wa Hajiri na Sara (Gal.4:22-31). Akirejea kwa wana wa Ibrahimu, anarudi kwenye mjadala wa Ahadi ambao aliuanza katika Wagalatia 3:6-29.

(Sasa unashauriwa kusoma Wagalatia 4:21-31 ambayo sitaijadili, juu ya Ushika-sheria wa Wana-Uyahudi).

WAGALATIA 5:1 : SHERIA YA UHURU

Hoja: Ikieleweka vema, Sheria ni sheria ya uhuru (Yakobo 1:25; 2:12). Kwa hiyo, Wana-Uyahudi hawawezi kuzuilia uhuru wa Kikristo wala Wana-Roho hawawezi kutumia uhuru katika kupinga amri za Mungu.

Wagalatia 5:1: “Katika ungwana huo Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa.”

Katika Wagalatia 5:13-14; Paulo anawaonya Wana-roho dhidi ya matumizi mabaya ya uhuru katika Kristo, katika mstari wa 1, anawaonya Wana-Uyahudi dhidi ya uzuiaji wa uhuru huo na kuugeuza kuwa kongwa. “Katika ungwana huo Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa.”

Sheria hutoa uhai, kwa kweli inaumba nafasi ya upumuaji ilio muhimu kwa uhai. Ni “sheria kamilifu iliyo ya uhuru” (Yakobo 1:25; 2:12), haizuii hatua za mtu (Mith. 4:12), ina “utanua moyo”. Baada ya uhuru wa Israeli kutoka Misri, “Watu walimhofia Bwana, na kumwamini Bwana na mtumishi wake Musa.” Ukweli kwamba Mungu alikuwa ameichagua Israeli kuwa watu wake chini ya Ibrahimu na kisha kuwakomboa kutoka katika utumwa wa Misri kabla ya kuwapa Sheria juu ya Mlima Sinai, ni wenye umuhimu mkubwa katika Agano la Kale. Utangulizi katika Amri Kumi za Mungu unadhihirisha hili: “Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri katika nyumba ya utumwa. Usiwe na…” (Kut. 20:2). Mambo ya Walawi 11:44-45 inahalalisha Amri maalumu sio tu katika utakatifu wa Mungu, bali pia katika kazi yake ya Ukombozi. “Kwa kuwa mimi ni BWANA, Mungu wenu; takaseni nafsi zenu basi; iweni watakatifu, kwa kuwa mimi ni Mtakatifu…Kwa kuwa mimi ni BWANA niliyewaleta kutoka nchi ya Misri, ili kwamba niwe Mungu wenu; basi mtakuwa watakatifu, kwa kuwa mimi ni Mtakatifu.” David Chilton anaandika, “Kutoka kuliwapatia Waisraeli uhuru na sheria.”[103] George Huntemann alilielezea hili kwa mtindo ufuatayo: “Amri inamwonesha mtumwa barabara kuelekea kwenye uhuru.”[104]

Kwa hiyo, yeyote anayeikataa sheria, hauiti uhuru, bali utumwa! Hata Mtheolojia Myahudi, Pinchas Lapide, anaandika katika utangulizi wake juu ya Amri Kumi,

> “Pasipo injili ya ukombozi ya Kutoka – hakuna Sinai ya Amri. Lakini pasipo Sinai na Amri zake – hakuna maisha ya kiimani yenye kutendeka.”[105]

George Downame (1560-1634), Askofu wa Derry na Kiongozi wa kiroho wa ibada za Mfalme wa Kiingereza, aliandika, “Tunakiri kuwa Mungu ametuweka huru kutoka katika laana na utumwa wa Sheria, ili tuwe na uwezo wa kumtii yeye katika uhuru wa Roho…[106]

(Sasa unashauriwa kusoma Wagalatia 5:2-5 juu ya Ushika-sheria wa Wana-Uyahudi, ambao sitaujadili.)

MAPITIO: JUU YA TOFAUTI KATI YA SHERIA YA MAADILI NA SHERIA YA MAADHIMISHO[107]

Katika Wagalatia 5:6, Paulo anafanya tamko la kushangaza juu ya tohara: “Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, bali imani itendayo kazi kwa upendo.” Anaelezea wazo sawa na hilo katika 1 Kor. 7:19: “Kutahiriwa si kitu, na kutokutahiriwa si kitu; bali kuzihifadhi amri za Mungu.” Je, hapingi mawazo mawili yanayofanana? Tohara ilikuwa moja ya amri za Mungu, kama zilivyo Amri Kumi, haikuwa hivyo?[108] Vifungu kama Wagalatia 5:6, 1 Kor. 7:19 na vingine vingi hudhihirisha mambo mawili:

1) Hata katika Agano la Kale, Mungu alikuwa ametaka zaidi ya matimizo ya nje ya amri zake. Wakristo wengi huamini kuwa katika Hotuba Mlimani, Yesu alikuwa akiitanua sheria ya ‘nje’ dhidi ya uzinzi, kwa sheria ya ‘ndani’ dhidi ya tamaa (Mat. 5:27-32). Hata hivyo, Amri Kumi, tayari zilijumuisha sheria ya “nje” dhidi ya uzinzi na sheria ya ‘ndani’, “Usimtamani mke wa jirani yako…”[109] Amri Kumi inaeleza mtazamo wa ndani wa sheria dhidi ya uzinzi (kumtaka mke wa mtu mwingine) na sheria dhidi ya uibaji (kutaka mali ya mtu mwingine).

2) Kwa uangalifu mkubwa, sheria ya maadili ya Agano la Kale, ambayo Amri Kumi zinaieleza kwa kifupi, zinaweza kutofautishwa na sheria ya maadhimisho, ambayo ilijumuisha taratibu juu ya dhabihu, utakaso na vyakula, na vilevile tohara.[110]

Sheria ya maadili ni halali kwa nyakati zote na itakuwa sheria itakayotumiwa kuwahukumu watu wote katika Hukumu ya Mwisho. Roho Mtakatifu huitimiza ndani ya Wakristo, kwa kuwa Kristo aliipatia utimilifu wake juu ya Msalaba (Ru.8:3-4, 13:8-10).[111]

Hata hivyo, sheria ya maadhimisho iliwahusu Waisraeli tu, na ilitimizwa na Kristo kama kitabu cha Waebrania kinavyodhihirisha, Yesu alitosheleza matakwa yake kikamilifu na kwa hatua ya mwisho, ili kwamba isihitajike kuendelea kufanywa. Sheria ya maadhimisho inabaki kuwa msingi halali wa kisheria kwa yote yaliyotokea Msalabani, kwa kuwa kama ilitanguliwa, umwagaji wa damu ungekuwa na umuhimu tena (Ebr. 9:22-24; Law.17:11)!

Wale wanaoshikilia sheria ya Agano la Kale kutokuwa na wajibu kwa Wakristo huona tofauti hizi kama za kubuni tu kwa kuwa Agano la Kale

lenyewe limezisokota pamoja. Hata hivyo, neno “Sheria” linahesabu sio tu taratibu za mtu binafsi, bali daima hutajwa kama Neno la Mungu (kwa mfano katika Zab. 19 na 119). Amri za mtu binafsi mara nyingi zinawekwa kwa ukaribu na ahadi na matukio ya kihistoria. Sio kwamba unabii uko katika hali ya ‘upekee’ katika Biblia, bali daima umeunganishwa na amri na habari za kihistoria.

Ninapata asili ya mgawanyo wa Sheria katika aina za maadili na maadhimisho si sana katika maandiko ya Mababa wa kanisa au Wana-matengezo, bali kimsingi katika Agano la Kale lenyewe (Zab. 40:6-10; Yer. 7:21-24) na katika Agano Jipya (1Kor. 7:19).[112]

Vifungu Ambavyo Vinatofautisha kati ya Sheria ya Maadili na Maadhimisho
Mithali 21:3" Kutenda haki na hukumu humpendeza BWANA kuliko kutoa sadaka ."
1Kor. 7:19 " Kutahiriwa si kitu, na kutokutahiriwa si kitu; bali kuzihifadhi amri za Mungu ."
Wagalatia 5:25 "Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, bali imani itendayo kazi kwa upendo ."
Warumi 2:25 " Kwa maana kutahiriwa kwafaa sana ukiwa mtendaji wa sheria, lakini ukiwa mvunjaji wa sheria kutahiriwa kwako kumekuwa kutokutahiriwa."
Waebrania 7:16 Ukuhani wa Yesu haukuazia katika *'amri iliyo ya jinsi ya mwili,'* kama ilivyokuwa katika ukuhani wa Agano la Kale*. Sheria ya maadhimisho inaelezwa kama 'amri iliyo ya jinsi ya mwili '* na inatofautishwa kutoka katika maagizo ya maadili.

Agano Jipya linatazama kwamba kifo cha kidhabihu cha Kristo Msalabani kimetimiza sheria ya maadhimisho kwa ujumla, ili kwamba pasiwepo hata moja ya taratibu zitakazohitajika kutekelezwa tena. Baba wa kanisa Aurelius Augustinus (335-430 BK.) aliandika:

> “Ninaamini kwamba tohara na maagizo mengine vilitolewa na Mungu katika Agano la Kale katika matarajio ya vitu vijavyo ambavyo vingetimizwa katika Kristo tu. Sasa hili limekwisha tokea, Wakristo ni lazima wazisome kwa jitihada na uangalifu, ili kuelewa utimilifu wake, hata hivyo, sio kwa ajili ya kuzitenda, kana kwamba ni muhimu…Ingawa Mataifa hawakupaswa kuzitii, (sheria hizi) zisingeweza kutanguliwa, kana kwamba zilikuwa mbaya sana na zenye kuchukiza…”[113]

WAGALATIA 5:6 NA 6:15 : SHERIA YA MAADHIMISHO KATIKA WARAKA KWA WAGALATIA

Hoja: Onyo ya kwamba tohara ya Mataifa ni ya ushika sheria inathibitisha kuwa Paulo mara nyingi anatumia neno 'sheria' katika Wagalatia sio kuonesha sheria ya maadili bali sheria ya maadhimisho, ikijumuisha tohara. Wana-Uyahudi walitaka kulazimisha sheria ya maadhimisho kwa Mataifa.

Wagalatia 5:6: "Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, bali imani itendayo kazi kwa upendo."

Wagalatia 6:15: "Kwa sababu kutahiriwa si kitu, wala kutokutahiriwa, bali kiumbe kipya."

Katika Wagalatia 5:6, neno 'kutahiriwa' linaashiria na kupinga kikundi cha Wana-Uyahudi, wakati neno 'govi' (kwa kawaida linatafsiriwa 'kutokutahiriwa') hurejea na kuwapinga Wana-roho.[114] Hii inaonesha na kuashiria kwamba baadhi ya washirika wa makanisa ya Galatia walijisifu kwa kutahiriwa kwao, wakati wengine walijisifu kwa kutokutahiriwa kwao. Paulo anasisitiza hili mwishoni mwa waraka wake (Gal.6:15).

Kama watoa-hoja (makomenteta) wengi walivyoonesha,[115] mtume anaupinga ushika-sheria na utunzaji wa sheria ya maadhimisho kwa Mataifa baada ya kifo na ufufuo wa Kristo, na sio utii wao kwa sheria ya maadili.

Christoph Haufe anathibitisha tofauti kati ya sheria ya maadili na ile ya maadhimisho kwa kuonesha kwamba Paulo anaiona 'sheria' iliyotanguliwa na kukataliwa kwa wale ambao wanajaribu kuishika, hivyo basi wanaanguka kutoka katika neema. Hata hivyo, katika waraka huu anaona kwamba Sheria ni lazima itimizwe (Gal.5:13-14) na haipingani na wale wanaosulubisha tamaa na mwili kwa nguvu za Roho (Gal.5:18, 22-24).[116]

> "Tofauti kati ya Mataifa na Wayahudi inaondolewa katika Kristo (Gal. 3:28; 1 Kor. 12:13; Rum. 10:12; Kol. 3:11). Tofauti hii haiweza kuendelea, kwa kuwa Mataifa na Wayahudi pia watahukumiwa kwa sheria ya maadili, ambayo wote wanaishiriki (Rum. 2). Sheria ya maadhimisho ambayo Kristo ameiondoa (Efe. 2:15), ni sheria

iliyowatofautisha waliotahiriwa na wasiotahiriwa (Efe. 2:11), sheria ya kidini ya Kiyahudi".

"Mahali Paulo anapokataa sheria katika Wagalatia, anazungumzia 'tohara' ya 'utakaso' au ya 'sherehe za kidini.'"[117]

C.E.B Cranfield anaandika katika mtiririko uleule:

"Tunatambua kutoka katika hili, Paulo hamaanishi Sheria yenyewe katika Wagalatia 4:3, 9, bali mtazamo potovu wa Washika-sheria na matumizi mabaya ya Sheria."[118]

Akiandika juu ya Wagalatia 4:10-11, Christoph Haufe anaonesha kuwa Paulo asingeweza kuandika, "Mnashika sheria dhidi ya wizi. Nawachelea, isiwe labda nimejitaabisha bure kwa ajili yenu!"[119]

WAGALATIA 5:7-12 : KUJIPENYEZA KWA UKOSA-SHERIA WA KIPAGANI, KWA KIWANGO CHA KUJIKATA BINAFSI

Hoja: Maelezo makali ya shitizai ya mstari wa 12, kwamba baadhi ya washirika wa Kanisa yawezekana wamejikatakata nafsi zao, hayarejei kwa tohara, bali kwa desturi za kawaida za kipagani za dini nyingi za Asia Ndogo, hususani dini ya kizushi ya Wasebele. Paulo asingeweza kuifanya kichekesho tohara ya Kiyahudi kwa mchezo wa maneno ya kebehi.

Wagalatia 5:7-12: “Mlikuwa mkipiga mbio vizuri; ni nani aliyewazuia msiitii kweli? Kushawishi huku hakukutoka kwake yeye anayewaita ninyi. Chachu kidogo huchachua donge zima. Nina matumaini kwenu katika Bwana, ya kwamba hamtakuwa na nia ya namna nyingine. Lakini yeye anayewafadhaisha atachukua hukumu yake, awaye yote. Nami, ndugu zangu ikiwa ninawahubiri habari ya kutahiriwa, kwa nini ningali ninaudhiwa? Hapo kwazo la msalaba limebatilika! Laiti hao wanaowatia mashaka wangejikata nafsi zao!”

Hili linalingana na muktadha? Ni kwa akina nani onyo la Paulo katika Wagalatia 5:9 linaelekezwa (“chachu kidogo huchachua donge zima.”)? Mistari hii inabaki kuwa migumu katika kuielewa, iwapo itatumika kuhusishwa na Wana-Uyahudi, lakini sio wakati itumiwapo kwa Wana-roho.[120]

Wana-roho waliiona dhambi, makosa dhidi ya sheria ya maadili, kuwa haina madhara. Hata hivyo, Paulo anashikilia hili kuwa kitisho hatari kinachokuwa katikati ya kanisa kama chachu. Walaghai wanapinga utii kwa amri za Mungu za milele.

Tamko thabiti la Paulo katika mstari wa 10, “Nina matumaini kwenu katika Bwana, ya kwamba hamtakuwa na nia ya namna nyingine” laonekana kupinga maoni yake ya jumla kwa Wakristo wa Galatia (Gal. 1:6, 4:16, 5:1, 6:12). Hata hivyo, ugumu unapotea wakati tufikiriapo kuwa Paulo anaelezea jaribu la Wana-roho, ambalo lilikuwa bado halijaota mizizi katika kanisa, kama ilivyokuwa nafasi ya Kiyahudi, ambayo tayari ilikuwa imekwisha pata ushawishi mkubwa,[121] na ambayo yeye anaiona kuwa isiyofaa kitu.

Mashtaka ya “kujikata” (‘mtu kujikata nafsi yake’) yanahitaji umakini wa kipekee. Kwa ujumla inatafsiriwa kama kichekesho cha tohara ya Kiyahudi. Lütgert anajibu:

“Paulo asingeweza kuifanya kichekesho tohara kwa kuilinganisha na kujikata nafsi, kwa kuwa hili lingekuwa ni aina ya uandishi wenye kebehi kali. Katika Wafilipi 3:5 yeye mwenyewe anakiri bila aibu kuwa ni mwenye kutahiriwa. Hakuna hata mara moja tu katika hali ya ushindani mkali juu ya suala hili alishafikiri kutilia mashaka sifa yake ya alama ya agano lililowekwa na Mungu.”[122]

Kama kifungu kinawahusu Wakristo Wana-roho wa Mataifa, basi neno ‘kujikata nafsi” linawezekana kurejea zaidi kwa “mtu mwenyewe kujikatakata kwa kuondoa sehemu ya viungo vya mwili wake kulikofanywa na dhehebu la kizushi la Wasebele.”[123] Hii ilikuwa ni hatua ya mwisho na ya hali ya juu kabisa ya furaha ya kiroho ya dini, ambayo ilisambaa katika eneo kubwa la Asia Ndogo na katika eneo la Galatia.

> “Katika Asia Ndogo kutajwa kwa upotokaji wa kidini ambao ungeweza kupanda hata kiwango cha kujikatakata nafsi, mawazo ya kujikatakata nafsi ya dini ya kizushi ya Wasebele kungefanywa tu kwa makanisa ya Kikristo ya Mataifa kwa kuwa ilikuwa ni zoezi la kujikata lililozoeleka zaidi kwao. Mwili wa Atisi uliaminiwa kutunzwa katika ujirani wa karibu kabisa na makanisa ya Pesinasi, mahali ambapo makuhani walimtumikia yeye na kufuata mfano wake kwa kujikatakata nafsi zao wao wenyewe. Katika Asia Ndogo, katika eneo la Galatia, toleo la Frigia lilitawala. Warumi pia waliona kitendo cha dini ya kizushi kujikatakata miili yao kuwa ni machukizo makubwa. Ilikuwa ni kiwango cha juu kabisa cha msisimko wenye vurugu kilichotafutwa na washiriki wake. Wakati tusikiapo majaribu ya kidini katika kanisa la Galatia, ikiwa jambo la kwanza mtu awezalo kulifikiri ni kujikata nafsi, basi dini ya kizushi ya Wasebele huja akilini haraka. Kwa hakika haikuwa makuhani wa dini bali ndoto zenye nguvu ya kiroho isiyoelezeka iliyochochewa na dini ya kizushi ambayo ilikuwa imejipenyeza ndani ya kanisa, na ilikuwa imepata kukubaliwa na Wana-roho. Sasa ni kwamba ilikuwa imeendelea kwa kiasi kikubwa, hivyo Paulo angeweza tu kusema, “Kitu kimoja tu kinapungua, ni lazima waanze kujikatakata miili yao wenyewe!” Kuenea kwa uzushi katika makanisa sasa kunajumuisha, uabudu sanamu wa nguvu ya kiroho isiyoeleweka ambao mtume anaupinga kwa nguvu. Ulikuwa umepata kukubaliwa na kundi la Wana-roho, ukayafurikisha makanisa kwa uchafu wa kipagani.”[124]

Albrecht Bengel na Wilhelm Lütgert wanayaunganisha maneno, “Ningeweza kutamani…” kwenye sentensi iliyotangulia, sio katika wazo

la kujikatakata nafsi.[125] Hivyo mstari unasomeka, “Natamani ingekuwa hivyo! Laiti hao wanaowatia mashaka wangejikata nafsi zao [au kujikatakata miili yao wenyewe].” Mgawanyo wa kijadi wa sentensi pia unaruhusu tafsri yetu ya kujikata nafsi.[126] (Tafsiri ya Kiswahili haikujumuisha kishazi hiki [kifungu hiki cha maneno, “Ningeweza kutamani…”] Tafsiri ya Kiingereza ina kifungu hicho, nacho kiko katika mstari wa 12. Kwa hiyo mwandishi anaonesha kuwa kilipaswa kuwa katika mstari wa 11, maelezo haya yaliyolazwa ni ziada ya mtafsiri).

WAGALATIA 5:11; 6:12 : SABABU YA MATESO

Hoja: Wana-Uyahudi walishurutisha kwamba Waamini wa Mataifa sio tu washike sheria yote ya maadhimisho, bali pia watahiriwe, ili waepuke mateso kutoka kwa Wayahudi.

Wagalatia 5:11; "Nami, ndugu zangu ikiwa ninahubiri habari ya kutahiriwa, kwa nini ningali ninaudhiwa? Hapo kwazo la msalaba limebatilika."

Wagalatia 6:12: "Wote watakao kuonekana ni wazuri kwa mambo ya mwili, ndio wanaowashurutisha kutahiriwa; makusudi wasiudhiwe kwa ajili ya msalaba wa Kristo, hilo tu."

Maana ya Wagalatia 5:11 ni lazima ichunguzwe katika muktadha wake pamoja na tafsiri ya sura ya 5 hapo juu, "Nami, ndugu zangu ikiwa ninahubiri habari ya kutahiriwa, kwa nini ningali ninaudhiwa?"[127]

Tafsiri nyingi hufundisha kuwa Paulo anadai kuteswa kwa sababu hahubiri tena tohara. Hata hivyo, yeye anasema kitu kingine kabisa, "ikiwa ninahubiri habari ya kutahiriwa, kwa nini ningali ninaudhiwa?" "Sio mateso yake, bali ujumbe wake ndio wenye kutiliwa mashaka."[128] Kwa kurejea mateso, Paulo anakanusha mashtaka kwamba yeye anahubiri kutahiriwa! "Ugumu wetu katika kuelewa msingi wa historia ya mashtaka hautupi haki ya kupinga kweli zilizoelezwa katika maneno dhahiri."[129]

Dai kama hilo ni vigumu sana kuweza kuwa na asili yake kutoka kwa Wayahudi, wakati Wana-roho wanaweza vema kuwa wametengeza mashtaka hayo. Wanadai, Paulo 'bado' anahubiri msimamo ulioshindwa zamani. Ukweli ni kwamba aliruhusu tohara, ingawa si muhimu kwa wokovu, na hata alimtahiri Tito (Mdo. 16:3) 'ulithibitisha' kwao kwamba Paulo yeye mwenyewe bado hajajiweka mbali na Sheria. Lütgert anaandika, "…Kusema ukweli, wale waliomhukumu kwa njia hii walikuwa ni wapinzani wake, kwao hakuwa Mtu Mpya, bali "Aliyerudi nyuma".[130]

Sababu za kihistoria za mgawanyiko katika makanisa ya Galatia zaweza kupatikana katika Wagalatia 5:11.[131] "Nami, ndugu zangu ikiwa ninahubiri habari ya kutahiriwa, kwa nini ningali ninaudhiwa? Hapo kwazo la msalaba limebatilika!"

> “Mateso ya Wakristo yaliyotajwa hapa yalianzishwa na Wayahudi. Kwa asili, Paulo hawezi kumaanisha mgogoro na Wana-Uyahudi, kwa kuwa wao wenyewe wametikiswa, hivyo basi wanajaribu kuepuka magumu kwa kuhubiri tohara, kama Wagalatia 4:29 inavyodekeza. Kama Ishmaeli alivyomtesa Isaka, wale waliozaliwa kwa mwili bado wanawatesa wale waliozaliwa kwa Roho.”[132]

Wagalatia 6:12 inadhihirisha wazi kwamba wasiotahiriwa waliteswa

> “Kadri wengi watamanivyo kufanya mwonekano mzuri katika mwili, 'haya yangewavuta ninyi kutahiriwa, ili tu wasiweze kuteswa kwa ajili ya msalaba wa Kristo.’ ‘Wayahudi waliwatesa Wakristo, kwa sababu walikuwa hawakutahiriwa…’ Gal. 3:4 hurejea kwenye suala hili pia. ‘Mmeteseka sana katika ubatili, ni tafsiri sahihi.”[133]

Paulo anarejea nyuma kuwa yeye mwenyewe alikuwa adui wa kanisa (Gal. 1:130), ambalo lilimsifu Mungu kwa kuongoka kwake (1:23-24). Sasa anasisitiza kwamba yeye mwenyewe ndiye anayeteswa, ili kukanusha mashtaka kwamba anahubiri tohara ili kuepuka mateso.

Wana-Uyahudi walijaribu kuanzisha tohara kwa waamini wa Mataifa ili kuepuka magumu kutoka kwa Wayahudi, ambao waliwachukia Wakristo wa Mataifa wasiotahiriwa na Wakristo Wayahudi waliovumiliana nao. “Hili tu laweza kuelezea tumaini la Wana-Uyahudi kwa mafanikio katika kujaribu kuwashawishi ndugu zao wa Mataifa kutahiriwa.”[134]

Kwa sababu hii, Wakristo Wayahudi walishurutisha tohara tu na sio kushika sehemu nyingine ya sheria ya maadhimisho. Paulo alipaswa kuweka wazi kwamba tohara pekee haitoshi, bali inaonesha utii kwa sheria yote ya maadhimisho, ikijumuisha dhabihu, kuosha, kalenda ya sikukuu, na pia sheria juu ya utakaso na juu ya vyakula.

WAGALATIA 5:13-26 : UHURU DANGANYIFU WA WASIO-SHERIA

Hoja: Mgogoro wa Paulo na Wana-roho wasio na sheria katika kanisa la Galatia unaonekana wazi zaidi katika Wagalatia 5:13- 26. Hapa, anawaonya dhidi ya matumizi mabaya ya uhuru wa Kikristo na anasisitiza kwamba Roho wa Mungu huzaa upendo tu, ulio kiini cha Sheria, na wala sio matendo ya mwili, ambayo yanaenda kinyume na Sheria.

Wagalatia 5:13-26: “Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tumikianeni kwa upendo. Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, Umpende jirani yako kama nafsi yako. Lakini mkiumana na kulana, angalieni msije mkaangamizana.

Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka. Lakini mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria. Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo; katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu. Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho. Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana.”

Kuwapo kwa kundi la pili katika kanisa la Galatia, lile la Wana-roho wasio-sheria ni wazi zaidi katika Wagalatia 5:13-14. Uhuru kutoka kwa Sheria ulioeleweka kimakosa huongoza kuelekea katika kutenda dhambi kinyume na mapenzi ya Mungu. “Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili…” (Gal. 5:13).

Ukinzani katika mstari wa 13 (na yawezekana katika mstari wa 1) unaelekezwa kwa Wana-roho wasio na sheria, ambao wanadai 'uhuru' waliomaanisha kuuelewa si uhuru wa kuondokana na uovu bali uhuru kuelekea uovu, kwa maadili yenye kuruhusu zinaa. Ukiri wa Matengenezo ya Westminster (The Reformed Westminster Confession) wa mwaka 1647 unafupisha onyo la kibiblia dhidi ya zinaa iliyovishwa uhuru katika Ibara ya 20:3,

> "Wale ambao, katika kujifanyia uhuru wa Kikristo, wanafanya dhambi yoyote, au kufurahia tamaa yoyote, hivyo basi wanaharibu mustakabali wa uhuru wa Kikristo ambao, ni kwamba, kukombolewa kutoka katika mikono ya adui zetu, ili tuweze kumtumikia Bwana pasipo hofu, katika utakatifu na haki mbele yake, siku zote za maisha yetu."[135]

Mstari wa 15 unaelezea mgawanyiko katika kanisa, "Lakini mkiumana na kulana, angalieni msije mkaangamizana!" Ni jambo lenye kufurahisha kuona kwamba tamko la kimafumbo la Paulo linafuata sentensi isemayo kwamba Torati yote inatimizwa katika upendo, "Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, Umpende jirani yako kama nafsi yako" (Gal. 4:14). Kwa Wana-Uyahudi, kwa asili hili linamaanisha kwamba kuishika Sheria kungeongoza kuelekea katika upendo. Hapa, Paulo anashambulia tafsiri potovu ya uhuru ambayo anaizungumzia katika mstari wa 13.

Kwanza Paulo anatamani kuwakumbusha Wana-Uyahudi wapinzani, wanaokataa Sheria kwa kigezo cha Roho, kwamba Roho wa Mungu daima huzaa upendo. Uhuru wa Roho hauwezi kutuongoza katika kukosa upendo na wema, kwa kuwa matunda yake huakisi upendo katika kila nyanja: "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi" (Gal. 5:22-23). Upendo hudhihirisha uvumilivu halisi, kiasi (uwezo wa kujizuia) na sifa nyinginezo. Kwa sababu aina hizi za upendo, kimaana haziwezi kwenda kinyume na Sheria, haraka Paulo anaongeza, "juu ya mambo kama hayo hakuna sheria." Kwa kuwa amri ya upendo ni roho ya Sheria, upendo huzaliwa na Roho wa Mungu na kuelezewa katika matunda yake, hauwezi kupingana na Sheria ya ki-Mungu.

Matunda ya Roho hukubaliana na Sheria ya Mungu, kama inavyoelezwa katika Amri Kumi (Gal. 5:14. Tazama pia Rum. 13:8-10, Gal. 5:18, 23). Matendo ya mwili, hata hivyo, ni makosa dhidi ya sheria ya Mungu na yamekwisha kutajwa katika Agano la Kale. "Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi,

husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu" (Gal.5:19-21).

Lütgert akijadili wito wa Paulo wa nafasi ya amri ya upendo kama kiini cha sheria ili kupinga upinzani dhidi ya Sheria anaandika:

> "Mstari wa 14 unarejea kwa hili, kwa kuwa unaonesha kwamba utimilifu wa Sheria na uhuru mbali na Sheria unaletwa kwenye makubaliano kupitia upendo, ambao ni sawa na uhuru na utimizaji wa Sheria. Hii inahusisha pande zote mbili, Wana-Uyahudi na vilevile Wakristo wazinzi. Hata hivyo, hapa Paulo anazungumza na wale waliotumia uhuru wao kwa kigezo cha kutosheleza mwili."[136]

Baada ya kutaja matunda ya Roho, Paulo anaongeza, "Juu ya mambo kama hayo hakuna sheria", ni vigumu kuwa anazungumza na Wana-Uyahudi, kwa kuwa wasingeweza kamwe kuyapinga hayo. Inaeleweka tu ikiwa yanaelekezwa dhidi ya wapinzani wa Sheria."[137]

> "Maelezo pekee yanaweza kuwa kwamba, kanisa lilitofautisha kati ya Sheria na Roho. Hapa tuna ulinganifu wa Warumi 7:7. Wapinzani wa Paulo hawako huru mbali na Sheria kama na yeye alivyo, lakini ni maadui wa Sheria na Wapinga-sheria. Hawaiamini sheria kuwa ni takatifu, njema na ya haki, au ya kiroho, kama Paulo alivyofanya, bali (waliiamini kuwa) ni ya kimwili na yenye dhambi. Hii haiwezekani, Paulo anasema, kwa kuwa haiyapingi matunda ya Roho."[138]

"Mwili" (Gal. 5:13, 15, 17, 19) humpinga Mungu daima na kila mahali; huasi dhidi ya amri zake, yeye ambaye alizipulizia pumzi na ambaye husaidia kuzitambua: "Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii" (Rum. 8:7). Ni kwa kuishi tu kwa Roho mtu aweza kushinda uasi huu na kuishi kwa upendo, ambao ni umuhimu wa kweli uliomo katika Sheria, "Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho" (Rum. 8:3-4). Yeye atembeaye katika Roho hutimiza matakwa ya Sheria, lakini si kwa nguvu zake mwenyewe, bali kwa kupitia nguvu za Roho na kwa kupitia neema tu iliyosababishwa na kifo cha kidhabihu cha Kristo juu ya Msalaba.

Sehemu nzima ya Wagalatia 5:13-26, inaelekezwa dhidi ya Wana-roho, kwa sababu wanapaswa kushauriwa mara mbili; sio tu kuishi kwa Roho, bali pia kutembea katika yeye (Gal. 5:16, 25). Wasikubali tu kipawa cha uzima wa milele, bali pia ni lazima wakidhihirishe katika maisha yao ya kila siku. Hii haiwezi kujumuisha matendo ya mwili yaliyozuiliwa.[139]

> “Paulo anahubiri uhuru mbali na sheria katika Roho, lakini hakubaliani na mawazo kuwa vitu hivyo viwili vinapingana. Msimamo wake juu ya Sheria na Roho ulizipinga pande zote mbili, Washika-sheria na vilevile Wana-roho.”[140]

WAGALATIA 6:1-10 : PAULO ANAWASIHI WASIO-SHERIA KUCHUKUA MIZIGO YA WENGINE NA KUFANYA MEMA

Hoja: Katika Wagalatia 6:1-10, Paulo anawasihi Wana-roho wasio-sheria kutimiza Sheria ya Kristo kwa kuchukua mizigo ya wenzao, kwa kuwa wanyenyekevu, kwa kujipima wenyewe na kwa kufanya mema, ili kurithi yatokayo kwa Roho.

Wagalatia 6:1-10: “Ndugu zangu, mtu akighafirika katika kosa lolote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe. Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo. Maana mtu akijiona kuwa kitu, naye si kitu, ajidanganya nafsi yake. Lakini kila mtu na aipime kazi yake mwenyewe, ndipo atakapokuwa na sababu ya kujisifu ndani ya nafsi yake tu, wala si kwa mwenzake. Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe.

Mwanafunzi na amshirikishe mkufunzi wake katika mema yote. Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho. Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio.”

Ili kujaliana na kusihiana kila mmoja, mtu ni lazima ajisihi na kujijali mwenyewe kwanza. Kwa ulinganifu Agano Jipya linasisitiza wajibu wa Mkristo kukubali kuwajibika kwa nafsi yake, kubeba mzigo wake, na wajibu wa kukubali kuwajibika kwa wengine na kubeba mizigo ya wengine. Wagalatia 6:1-5 hurejea kwa mitazamo yote miwili ya ushauri. Umuhimu wa kuchukua mizigo ya wengine, na uhitaji wa kubeba mzigo wako mwenyewe hautupilii mbali zaidi ya kumaanisha kila mmoja.

Mitazamo yote miwili ilikuwa mipya kwa Wana-roho. Hawakutaka kujiweka chini ya sheria ya upendo kwa kuwachukulia wengine mizigo, kwa kuwa hiyo ingeweza kuzuia uhuru wao wenyewe, wala hawakuwa tayari kujichunguza kwa kina au kuyajali maisha yao wenyewe, kwa

kuwa hili lingewalazimisha kukubali amri za ki-Mungu kama sifa kwa matendo yao, tena ingepunguza kile walichokuwa wanakiita uhuru wao.

Wakristo Wana-roho wa Mataifa wale waliojiona kuwa ni wakamilifu, wanachorwa kama watu wasiofaa (Gal. 6:1). Kama ilivyo katika Korintho, ubinafsi wao ulijieleza wenyewe katika kushindwa kwao kuwahudumia walimu wao (Gal. 6:6, 1 Kor. 9:11-14),[141] hivyo basi, Paulo lazima awasihi, “Mwanafunzi na amshirikishe mkufunzi wake katika mema yote.”

Tena anawaonya kutotumia vibaya sababu za uongo za uhuru ili kuyaona maisha yao ya kimwili kuwa ni ya kiroho kwa njia ya kipekee, “Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele” (Gal. 6:7-8. Tazama pia Yakobo 3:18, 2Kor. 9:6, Ebr. 6:7-8). Badala yake, ni lazima watende mema, jambo ambalo Paulo analisisitiza mara mbili: “Tena tusichoke katika kutenda mema, maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho. Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio”, ambayo ilijumuisha washiriki wa kundi jingine. Kutenda mema kutaongoza kuelekea kwenye mavuno ya kiroho (Gal. 6:9-10).

WAGALATIA 6:2: SHERIA YA KRISTO INAWAFUNGA PIA WASIO-SHERIA

Hoja: Sheria ya Kristo ni sheria ya maadili ya Mungu inapotafsiriwa vema katika Kristo.

Katika Wagalatia 6:2 Paulo anawasihi Wana-roho wasio-sheria kuishika "Sheria ya Kristo": "Mchukuliane na kutimiza hivyo sheria ya Kristo…" Ili kuelewa tamko hili tutachunguza maelezo linganifu katika Agano Jipya.

Gerhard Friedrich amegundua kwamba maelezo, "sheria ya imani" katika Warumi 3:27 hayamaanishi 'mtindo wa asili' bali inaeleweka vema kama Sheria ya Agano la Kale, katika maana yake pana kama maagizo ya Neno la Mungu.[142] Wagalatia 6:2, Warumi 8:2 na 1 Wakorintho 9:21 pia vinarejea kwa Sheria ya Mungu, inatafsiriwa vema katika Kristo Yesu na kutimizwa katika yeye.

Katika Warumi 8:2 na katika Warumi 7:22-23, Paulo anakinzanisha 'sheria' mbili, "sheria ya dhambi na mauti" na "sheria ya Roho wa uzima". Kuyaelewa maneno haya kwa kulinganishwa na sheria za asili kama mitindo ya chanzo na matokeo, hakutendi haki kwa umuhimu wake. Kwa makusudi Paulo anachagua neno lililo sawa na "sheria" ambalo alilitumia hapo awali kumaanisha Neno la Mungu lililoandikwa. Je, Paulo hamaanishi uwezekano wa aina mbili wa kuitikia Sheria: kwa upande mmoja, jaribio la kushika Sheria kwa uwezo wa mtu mwenyewe, ambalo huongoza kwenye dhambi na kifo; na katika upande mwingine, kujazwa na Roho wa Mungu, ambaye anatimiza Sheria ya Mungu ndani yetu, kama Paulo anavyoeleza katika Warumi 8:4-8? Neno la Mungu likieleweka vema, kujumuisha na Sheria ya maadili, basi linakuwa "Sheria ya Roho wa uzima."

Vifungu mbalimbali ambavyo vinazungumzia "Sheria ya Kristo" au sheria "Yake' au "Yangu" (yaani Yesu), vinadhihirisha wazi kwamba Sheria inaweza kueleweka inapohusishwa na Yesu, na kwamba yaweza kutimizwa katika yeye tu, lakini pia ni kwamba hatuwezi kuwa na Kristo pasipo sheria yake? Clement wa Alexandria (155-220 B.K.) aliweza kuandika, "Kwa hiyo tutamkubali Kristo kama Sheria".[143] Ninaamini "Sheria ya Kristo' ni Sheria ya Maadili ya Mungu iliyotimizwa na kutolewa na Kristo. Ni kwa sheria gani maalumu ya Yesu ambayo

ingemaanishwa, ikiwa si amri za Mungu, kama zijitokezavyo katika Maandiko? Je, Yesu mwenyewe hatutazamishi kwenye Sheria ambayo Mungu alikuwa amekwisha kuitoa, wakati atangazapo amri zake?

" Sheria ya Kristo " na " Sheria ya Imani " n.k. katika Agano jipya[144]
"Sheria ya kristo" au " Sheria ya Imani " n.k.
Warumi 3:26-27:-" ...mwenye kumhesabia haki yeye amwaminiye Yesu. Ku wapi, basi, kujisifu? Kumefunguwa nje. Kwa sheria ya namna ngani? Kwa sheria ya matendo? La ! Bali kwa sheria ya imani ". Warumi 8:2 :-" Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti " .
Sheria ya Kristo
1 Wakorintho 9:21:-"...(si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo)". Wagaratia 6:2:-" Mchukuliane mizigo na kutimiza hivyo sheria ya Kristo ".

" Amri Zangu " na " Amri Zake "

(yaani Amri za Yesu)

Yohana 14:15 :-"Mkinipenda, mtazishika amri zangu ".

Yohana 14:21 -24:-"... mtu akinipenda ,atalishika neno langu ; na baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake . Mtu asiyempenda, yeye hayashiki maneno yangu, nalo neno mnalo lisikia silo langu, ila ni lake baba aliyenipeleka ".

Yohana 15:9-10,12:- "(inafuata baada ya mfano wa Mzabibu)". Kama vile baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake...Amri yangu ndiyo hii, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi".

1 Yohana 5:2-3:- "Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake, wala amri zake si nzito".

1 Yohana 2:3-5:- " Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake , ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye ashikaye neno lake , katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua kuwa tumo ndani yake" .

1 Yohana 3:23-24:-" Na hii ndio amri yake, kwamba tuliamini jina la Mwana wake Yesu Kristo, na kupendana sisi kwa sisi, kama alivyotupa amri. Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye, naye ndani yake".

> "Wakati Paulo asemapo, "Si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Mungu" (1 Kor.9:21), anakanusha uhalali wa hoja kwamba hakuna sheria yoyote zaidi kwa Wakristo. Paulo anazungumzia matarajio ya kimaadili na uhalali wake zaidi kuliko msamaha wa dhambi."[145]

Mtu aweza kupinga kwamba maelezo, "Sheria ya Kristo" hudokeza Sheria ya Upendo. Hata hivyo , Sheria hii haiipingi Torati, bali ni ufupisho wake,[146] kama Paulo anavyosisitiza, "…bali tumikianeni kwa

upendo. Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, umpende jirani yako kama nafsi yako" (Gal. 5:13-14).

Eckhard Schnabel anafupisha vema hitimisho la Paulo katika maelezo yake marefu na anaiona "Sheria ya Kristo" kuwa ni "Torati" (jina la Kiebrania kwa sheria ya Agano la Kale) ikieleweka vema:

> "Kwa Paulo, Sheria imepoteza umuhimu wake wote wa wokovu kwa kifo na ufufuko wa Kristo. Hoja za utetezi dhidi ya wapinzani Wana-Uyahudi waliokataa kulikubali jukumu la kipekee la wokovu la Kristo wakitaka kuendeleza utii kwa Torati kama jambo muhimu kwa wokovu zaweza kumwongoza Paulo kutoa matamko kanushi kuhusu Torati (hususani katika Wagalatia). Hata hivyo, Paulo haonei shaka asili ya ki-Mungu ya sheria wala endelezo lake halali kama ufunuo wa mapenzi ya Mungu. Kimsingi, Sheria imefikia mwisho wake kuhusu kazi yake ya uhukumu na kuhusu matumizi yake yasiyofaa kama njia ya kujipatia haki. Kristo amechukua juu yake mwenyewe hukumu ya dhambi za ulimwengu na ameleta haki kwa wale wote ambao wanaunganishwa naye. Kwa hiyo, Kristo ni mwisho (telos) wa Torati. Hivyo basi, Torati inatafsiriwa na kuthibitishwa na Kristo kama 'sheria ya Kristo'. Kwa mfuatano, kwa kufuata kusulubiwa sheria inakuwa kipimo na kiwango cha maisha ya kikristo, yakitimizwa katika ufalme wa Roho ambaye humbadilisha mwamini aliye kiumbe kipya 'katika Kristo', na katika ufalme wa imani. Kristo ndiye kituo cha uhakiki na kiini muhimu sana cha Torati. Hata hivyo, Kristo hana mahusiano ya kifunuo au kiasili na Sheria. Torati ni, na inaendelea kubaki kuwa 'Sheria ya Mungu'.[147]

WAGALATIA 6:11-18: KUTOKUWA SAWA KWA KUNDI LA WASHIKA-SHERIA

Hoja: Mwishoni mwa waraka wake, Paulo anawaonya tena Wayahudi washika-sheria dhidi ya kuiweka tohara kuchukua mahali pa Msalaba wa Kristo. Anarudia upya mashtaka yake kwamba hawako sawa, kwa sababu hawatunzi sheria yote ya maadhimisho, bali tohara tu, ambayo wameifanya kuwa ni jambo la lazima.

Wagalatia 6:11-18: “Tazameni ni kwa herufi gani kubwa nimewaandikia kwa mkono wangu mimi mwenyewe! Wote watakao kuonekana ni wazuri kwa mambo ya mwili, ndio wanaowashurutisha kutahiriwa; makusudi wasiudhiwe kwa ajili ya msalaba wa Kristo, hilo tu. Kwa maana hata wao wenyewe waliotahiriwa hawaishiki sheria, bali wanataka ninyi mtahiriwe, wapate kuona fahari katika miili yenu. Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu. Kwa sababu kutahiriwa si kitu, wala kutokutahiriwa, bali kiumbe kipya. Na wote watakaoenenda kwa kanuni hiyo, amani na iwe kwao na rehema, naam, kwa Israeli wa Mungu.

Tangu sasa mtu asinitaabishe; kwa maana ninachukua mwilini mwangu chapa zake Yesu.

Ndugu zangu, neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zenu. Amina.”

Daima Paulo anawawasilisha Wana-Uyahudi kama wasiofuata walichokisema awali, “Kwa maana hata wao wenyewe waliotahiriwa hawaishiki sheria, bali wanataka ninyi mtahiriwe, wapate kuona fahari katika miili yenu” (Gal. 6:13). Wanadanganya kanisa juu ya uzingativu wa matakwa ya Sheria, kwa kuwa wao wenyewe hawaitii (Ga. 6:13; 5:3).[148]

Tumekwisha jadili Wagalatia 6:12, ambayo kwayo Paulo anaelezea mateso na ukwepaji wa Wana-uyahudi kutoka kwenye mateso kwa msisistizo wao kwamba waamini wa Mataifa ni lazima watahiriwe.

MAPITIO : IMANI ZA USHIKA-SHERIA[149]

Hoja: Paulo katika kuonya dhidi ya ushika-sheria hapingi kutimiza amri za Mungu katika imani, bali kutozielewa vema kama njia ya wokovu, kuwalazimisha waamini wa Mataifa kushika sheria ya maadhimisho, au kujaribu kushika Sheria mbali na Kristo.

Kwa haraka haraka 'Ushika-sheria' unakuwa msemo utumikao kumwona yeyote anayetetea Sheria ya Biblia kuwa ni mwenye makosa. Hivi, hili ni neno la kibiblia? Je, Andiko huelezea ukinzani huo? Kwa kuwa neno lenyewe - linalolingana na neno la Kigriki au Kiebrania halionekani kwenye Biblia, wale wanaolitumia kama neno la kuwalaumu wengine wanapaswa kulifasili kutoka katika kiini cha Biblia.

Ingawa mimi binafsi ningependelea kuliondoa neno hilo kutoka katika msamiati wetu, ninaweza kukubali kuliwekea mipaka kwenye maana lililopewa na Mababa wa Kanisa, "jitihada kupata haki kwa matendo ya sheria". Hata hivyo, hivi sivyo limaanishavyo daima, na wala siyo maana yenye kufaa.

Gordon H. Clark anadhani kuwa katika historia ya kanisa 'Ushika-sheria' daima umemaanisha matarajio kwamba Mwanadamu angeweza kujipatia wokovu kwa kushika Sheria.[150] Kinyume chake kingekuwa ni haki kwa imani, ambayo hutuongoza kwenye utii sahihi wa Sheria. Clark anaendelea,

> "Katika karne ya sasa neno 'ushika-sheria' limechukua maana mpya. Elimu maadili ya mazingira hupuuza sheria na taratibu. Mtu yeyote ambaye kwa uelewa hutii sheria za Mungu huitwa mshika-sheria. Kwa sababu hii, Joseph Fletcher anakubaliana na uvunjaji wa amri yoyote katika Amri Kumi, na hivyo anaipeleka maana iliyo kinyume ya 'Ushika-sheria' kwa maadili ya kihistoria ya Uprotestanti."[151]

Ni jambo baya kwa kuwa hii ni kweli sio tu kwa Elimu Maadili ya Mazingira bali pia kwa Wana-asili wanaoamini Sheria kuwa imekwisha tanguliwa na kisha wanatangaza mfumo wowote wa kimaadili ujengwao juu ya Ushika-Sheria. Hata hivyo, Ushika-sheria hauwezi kushindwa na Ukosa-sheria. Greg L. Bahnsen anaandika.

> "Jibu kwa ushika-sheria sio uamini rahisi, uinjilisti pasipo hitaji la kutubu, ufuataji wa baraka ya pili iliyofichika katika Roho, au maisha ya kikristo pasipo maagizo ya haki na uongozi. Uelewa wa kibiblia

> unapinga ushika-sheria kwa kutumia ‘maisha ya kweli katika Roho’. Katika kuishi hivyo, Roho wa Mungu ni mwanzilishi wa maisha mapya mwenye neema, ambaye hutuhakikishia dhambi zetu na hatari mbaya dhidi ya sheria ya Mungu iliyovunjwa, ambaye hutuunganisha sisi na Kristo katika wokovu ili tuweze kushiriki maisha yake matakatifu, ambaye anatuwezesha kuelewa uongozi tuliopewa wa neno la Mungu, na ambaye hutufanya tukue katika neema ya Mungu ili tuwe watu ambao tunazishika vema amri za Mungu.”[152]

Alfred de Ouervain anaandika kwa msisitizo ule ule,

“Imekwisha kusemwa kwamba kushikamanisha matendo yetu kwenye Andiko huunda ushika-sheria, yaani mtu yuko huru na ushika-sheria wakati anapoipa nafsi yake sheria. Kweli, yeyote ambaye katika majivuno yake hutumia Sheria kwa kulingana na mawazo yake binafsi anatenda kwa jinsi ya ushika-sheria. Hii ni hali kwamba ama anakusudia kushika herufi za sheria au anatupilia mbali sheria iliyoandikwa na kuimarisha sheria zake mwenyewe.[154]

> Kamwe, Biblia si ya ushika-sheria. Hakuna mtu yeyote anayejipatia amali kutoka kwenye Neno la Mungu anayeonekana ni mshika sheria. Hata pasipo kuitumia kanuni katika mfumo wake wa kimaadili, Emil Brunner alilieleza hili vema, [154]

“Kama ilivyo Andiko pasipo Roho ni Uothodoksi (ushika imani zenye kukubalika na wengi tu), na Roho pasipo Andiko ni upinga-sheria na ushika dini sana bila akili.”[155]

Ushika-sheria usitumike kama msemo dhidi ya wale wanaorejea kwenye amri za Mungu, bali ni lazima utafsiriwe kulingana na Biblia na kisha upingwe kwa njia hiyo hiyo. Mtu ni lazima atafsiri ushika-sheria kumaanisha matumizi yasiyofaa ya Sheria, kisha ni lazima aweke wazi kutoka katika Andiko kile kinachomaanishwa na matumizi mabaya ya Sheria na jinsi Sheria inavyopaswa kutumiwa. Majedwali yafuatayo yanaorodhesha mitindo mitano ya ushika-sheria na matumizi matano sahihi ya Sheria.[156]

Ushika - sheria ni nini?

Agano jipya huelezea njia tano za matumizi ya sheria yasiyofaa:

1. Kushika sheria ili uhesabiwe haki na uokolewe (Tazama Rum.3:21-4:25; Efe 2:9-10).
2. Kulazimisha sheria ya maadhimisho kwa wengine (Gal 4:9-11; Kol.2:16-17, kitabu cha Waebrania).
3. Kuongeza sheria ya mapokeo ya kibinadamu kwenye sheria ya Mungu (Mk.7:1-15; Mt 15:1-9).
4. Kusahau mambo ya msingi kwa kupendelea mambo madogo madogo (Mt. 23:23).
5. Kujihusisha na utii wa nje wa sheria ya Mungu (Mk.7:18-23, Mt. 15:15-20, Mt. 23:27-28).

:

kile ambacho Ushika -sheria sio

Agano jipya halihukumu yafuatayo:

1. Kufikiri kuwa sheria ya Mungu ya maadili ni njema sana, ya haki, takatifu na ya kiroho (Rum. 7:12,14; 1Tim.1:8. Linganisha Zab.19:8-12; Zab.119).
2. Kutamani kushika amri za Mungu za maadili katika roho ya uana (sio katika roho ya utumwa) na katika nguvu za Roho Mtakatifu (Rum. 8:2-4;3:31).
3. Kuwasihi wengine kwa msingi wa sheria ya Mungu, wakati hili lifanywapo kwa nia iliyo sawa (Efe. 6:1-4).
4. Kutoa wito wa kushika sheria ya Mungu ya maadili (Yak.2:6-12; Rum.13:8-10).
5. Kutekeleza nidhamu ya Kanisa (Gal.5:18-23; 1 Tim.1:5 -11).

Katika muktadha huu, Edward Bohl, Profesa wa udogma kutoka Vienna, anasisitiza umuhimu wa Sheria ya Mungu kwa Wakristo, kwa

kuwa ni Sheria ya Mungu tu itoayo mwongozo kwa kuonesha sheria za uongo na mapokeo:

> “Hatuwezi kutupilia mbali Sheria kutoka katika uhusiano uliopo katika Kristo kati ya Mungu na mwamini: twaweza tusitafute taratibu mpya kwa matendo yetu au, kweli, kuinua mabadiliko ya mawazo yetu yasiyo na sababu juu ya heshima ya Sheria. Hatujakombolewa kuishi kwa namna ya Sheria maalumu za kimaadili au mafundisho ya ukamilifu, bali kutimiza Sheria ya Mungu (1 Kor. 7:19; Gal. 5:6; Rum. 8:4, 13:10). Andiko hufundisha wazi kuwa mwamini ni lazima atunzwe kwa kufuata njia ya kujitakasa kwa Roho Mtakatifu, lakini (Roho Mtakatifu) anatumia neno la Mungu, hususani Amri Kumi kama kipimo na sheria ya maisha yetu.”[157]

Bohl pia anapinga Uzamo (Upayatisti) kwa tabia yake ya kuunda sheria mpya ili kuchukua mahali pa Sheria ya Kibiblia inayoipinga:

> “Uzamo (Upayatisti) ulikumbwa na hofu hii wakati ulipofanya kuhesabiwa haki kuwa kigezo cha utakaso; kwa hiyo utakaso ulionekana kuwa mwendelezo wa kuhesabiwa haki, ambako kulipaswa kujidhihirisha katika utakaso. Uthibitisho huu wa imani kwa matendo mema uliongoza kuelekea kwenye sura tofauti kabisa pamoja na alama za imani ya mtu kuliko zile za Sheria ya ki-Mungu. Uhalisia wa kuhesabiwa haki ulijaribiwa kwa kipimo kingine zaidi ya kile cha Sheria ya Mungu. Mtu alitengeneza aina ya sheria mpya (nova lex), kwa ajili ya mwamini wa kweli.”[158]

KIAMBATISHO: ULINGANIFU WA WAGALATIA NA WARAKA KWA WARUMI

Waraka kwa Warumi kama mchakato wa Agano [159]
Jedwali lililochorwa kuonyesha matumizi ya neno "Hasha!"
A. Inayozidi kawaida au mpaka (Warumi 3:3-4)
"Basi, ikiwa baadhi yao hawakuamini? Je! Kutokuamini kwao kutaubadili uamiinfu wa Mungu? Hasha! Mungu aonekane kuwa amini na kila mtu mwongo;kama ilivyo andikwa...;(Rum.3:3-4).
B. Ngazi/Cheo (Rum.3:5-6)
"Lakini, ikiwa udhalimu wetu waithibitisha haki ya Mungu ,tuseme nini? Je, Mungu ni dhalimu aletaye ghadhabu? (Nasema kwa jinsi ya kibinadamu.) Hasha! Kwa maana hapo Mungu atawezaje kuuhukumu ulimwengu?" (Rum3:5-6).
C. Maadili (Rum.3:31-5:21)
"Basi, je; Twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! Kinyume cha hayo twaithibitisha sheria "(Rum.3:31).
D. Kiapo/ Ukiri (Rum 6:1-4)
" Tusema nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?" (Rum.6:1-3).
E. Urithi (Rum.6;15-7:6)
"Ni nini basi? Tufanye dhambi kwa sababu hatuwi chini ya sheria bali chini ya neema? Hasha! Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti,au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki" (Rum 6:15-16).

Mtindo wa Rejea au Kurudi kinyumenyume
E. Urithi (Rum.7:7-12)
"Tusemeje, basi? Torati ni dhambi? Hasha! Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria; kwa kuwa singalijua kutamani, kama torati isingalisema, Usitamani" (Rum.7:7)
D. Kiapo/Ukiri (Rum.7:12-9:13)
" Basi torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema . Basi je! Ile iliyo njema ilikuwa mauti kwangu mimi? Hasha! Bali dhambi, ili ionekane kuwa ni dhambi hasa, ilifanya mauti ndani yangu kwa njia ya ile njema, kusudi kwa ile amri dhambi izidi kuwa mbaya mno "(Rum. 7:12-13).
C. Maadili (Rum.9:14-10:21).
"Tuseme nini basi? Kuna udhalimu kwa Mungu? Hasha! Maana amwambia Musa, Nitamrehemu yeye nimrehemuye, nitamhurumia yeye nimhurumiaye" (Rum.9:14).
B. Ngazi/Cheo (Rum.11:1-10).
"Basi, nauliza, Je! Mungu aliwasukumia mbali watu wake Hasha! Kwa kuwa mimi nami ni Mwisraeli, mmoja wa wazao wa Ibrahimu, mtu wa kabila ya Benyamini.Mungu hakuwasukumia mbali watu wake aliowajua tokea awali..."(Rum.11;1-2).
A. Urithi (Rum.11: 11-16).
"Basi nasema, Je! Wamejikwaa hata waanguke kabisa? Hasha! Lakini kwa kosa lao wokovu umewafikia mataifa, ili wao wenyewe watiwe wivu" (Rum.11:1).

Hoja: Waraka kwa Warumi, kama ulivyo waraka kwa Wagalatia, unawapinga wote kwa pamoja, Wana-Uyahudi, waliotafuta wokovu kwa matendo na Wakristo wa Mataifa waliokataa sheria ya maadili ya Mungu na wao wenyewe kujiweka mbali kabisa na dini ya kiyahudi.

Mara nyingi Wilhelm Lütgert amedhihirisha kwamba kimsingi, maandiko mengi ya Agano Jipya yanaelekezwa dhidi ya upinga-sheria na kuwapinga wale waliochukua hitimisho danganyifu kutoka kwenye mafundisho ya wokovu kwa neema, kwamba kipimo cha Mungu cha maadili kimebadilika.[160] Tumekwisha kuona tafasili yake juu ya Wagalatia. Katika somo jingine bora kabisa,[161] ameonesha kuwa Waraka kwa Warumi pia unajishughulisha na mitazamo mingi potovu kwamba waamini wa Mataifa walishikamana na Agano la Kale na Israeli. Otto Michel anafupisha:

> “Kwa mujibu wa W. Lütgert…ni makosa kutafsiri Waraka kwa Warumi katika muktadha ulio kinyume na Uyahudi tu. Hotuba nyingi (Mfano, Rum. 3:31, 8:31, 13:8-10) hufundisha tathmini chanya ya Sheria na haziwezi kuelezwa katika msingi ulio kinyume na Uyahudi. Zaidi, inawezekana kwamba Paulo alipaswa kuukabili upinga-sheria wa Mataifa. Kweli, Paulo anaonekana kusumbuliwa na mashaka ya kuwa yeye mwenyewe ameendeleza zaidi upinga-sheria (Rum. 3:1-8). Dhana kwamba Warumi 6 inaelekezwa dhidi ya tabia ya wana-uhuru, kwa ujumla inakubalika. Warumi 9-11 pia zinakuwa wazi zinapoeleweka katika muktadha wa kihistoria, na kuchukulia kwamba hadhira ya Paulo ilikuwa kinyume na ukristo wa Kiyahudi ambayo kwa kiburi iliidharau Israeli.”[163]

Lütgert anafupisha matokeo yake:

> "Kimsingi, Waraka kwa Warumi ulikusudiwa kulinda kanisa la Mataifa katika Rumi dhidi ya ukristo wa wapinga-sheria. Ambao ulijumuisha dharau kwa Israeli na ushika-sheria wa Kiyahudi, na kwa wakati uleule kuchochea tabia za kimapinduzi katika kanisa. Ukristo huu ulisambaa miongoni mwa makanisa, ukirejea kwa Paulo kama mamlaka yake, lakini tayari ukianza kumpinga. Hivyo basi alikuwa na sababu ya kulinda Injili yake dhidi ya udogma huu, kulionya kanisa la Kirumi dhidi ya Injili, na kuhakikisha upokezi muhimu wa kazi yake katika Kanisa la Rumi. Matokeo yake ni kwamba, kwa maelezo anachukua msimamo chanya juu ya Sheria, na anawasilisha mafundisho yake ya Neema katika mtindo wa mafundisho ya kuhesabiwa haki, hivyo anaunganisha mtazamo wake chanya juu ya Sheria na mafundisho ya neema…Paulo

> alipaswa kulinda Sheria na Ukristo wa Kiyahudi dhidi ya waamini wa Mataifa."[164]

Uthibitisho wenye nguvu wa hitimisho la Lütgert kuwa Warumi hupinga dharau dhidi ya Sheria (Upinga-sheria[165]) na dharau kwa Israeli (Upinga-Uyahudi[166]) ni uchunguzi wa Ray R. Sutton wa muhtasari wa Warumi 3-11.[167] Paulo analinganisha waraka wa Paulo na mtindo wa Agano katika Agano la Kale,[168] ambao katika huo Paulo anaupitia mara mbili, kwanza katika mtindo wa kinyumenyume (rejea), ambao waweza kuonekana katika marudio ya kiapo "Hasha!"[169] (au "hilo haliwezekani kabisa!" au kimaandishi, "hilo haliwezi kutokea!") ambao unatambulisha maswali ya kujihoji ya Paulo. Hivyo Israeli inaitwa kwenye hukumu, kwa kuwa Injili ya Agano Jipya inakubaliana na Sheria ya Agano la Kale. Wakati uleule Mataifa wanakatazwa kutolijali Agano la Kale na Sheria. Maelezo, "Hasha!" ni kiapo,[170] kitu kilichotumika kuidhinisha maagano ya Agano la Kale, ambacho kilithibitisha sifa ya Agano ya Kitabu cha Warumi na msisitizo wake juu ya endelezo la uhalali wa sheria ya maadili ya Agano la Kale.

REJEA ZA NUKUU

1. Cornelius Van-derWaal, *Search the Scripture*, Vol. 8, *John-Romans*, (St. Catherines, Canada: Paideia Press, 1978), uk. 81. Ulinganifu wa maneno katika nyaraka za Paulo kwa kuanzia kubwa kwenda ndogo: maneno Rum: 7100, 1 Kor: 6800, 2 Kor: 4600, Efe: 2400, Kol: 1750, Flp: 1700, 1 Thes: 1550, 2 Thes: 850. Nyaraka kwa watu binafsi ni fupi zaidi.

2. Angalizo moja la kipekee. Waraka mfupi kabisa wa Paulo, Filemoni, unajishughulisha na jambo moja tu.

3. Tazama sehemu ya mwisho ya kitabu hiki, na vilevile Lütgert, *Römerbrief,* na Schirrmacher, *Römerbrief 1+2*, hususani Vol. 1, kr. 32ff, 280-281, 291-294, na Vol. 2, uk. 14-53, 242-262.

4. Lütgert, Gesetz und Geist, uk. 39.

5. Tazama Werner Neuer, "Wichelm Lütgert: Eine kleine Einfuhrung in Leben und Werk eines vergessenen Theologen", Jahrbuch *fur* evangelikale theologie 1 (1987), kr. 108-124.

6. Lütgert, Gesetz und Geist. Tazama pia Fuller, *Unity*, kr.459-480.

7. Tazama Schirrmacher, *Ethik 2*, kr. 34-47 kwa ajili ya uwasilishaji na ufupisho wa hoja za Lütgert.

8. James Hardy Ropes, "The Singular Problem of the Epistle to the Galatians", *Havard Theological Review* 14 (1929).

9. Frederic R. Crownfield, "The Singular Problem of the Dual Galatians", *Journal of Biblical Literature 64*, (1965) kr. 491-500).

10. F. F. Bruce, *Commentary on Galatians in New International Greek Commentary* (1982), repr. Exeter, G. B. Paternoster Press; Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans, 1992), kr. 23-25. Linganisha (na wasilisho kanushi) la historia la tafsiri ya Lütgert la Waraka kwa Wagalatia. Bruce anamwongeza kwenye mlolongo Johannes Munck, *Paulus und die Heilsgeschichte,* Acta ajutlandica: Aarsskrift for Aarhus Universiitet XXVI *(Ejnar Munks-gaard,* Kopenhagen: 1954), uk. 79-126; Kiingereza: *Paul and the Salvation of Mankind,* (London, 1959). uk. 87kk. Munck amejitenga mwenyewe kutoka kwa Lütgert, hata hivyo, pasipo kufuata tafsiri ya kimapokeo. James Hardy Ropes, Frederic R. Crownfield na

Johannes Munck wameliendeleza zaidi wazo la Lütgert, na kudhani kwamba Wana-Uyahudi walikuwa Waamini wa Mataifa. "Wana-Uyahudi wapinzani katika kitabu cha *Wagalatia ni Watu wa Mataifa"*, anasema Munck, *Paulus und die Heilsgeschichte,* uk. 79. Kwa mujibu wa msimamo huu, makundi yote mawili pinzani katika kanisa la Galatia yalikuwa ya wa Mataifa. Hoja kuu ni hii Wana-Uyahudi wazushi walitaka kutahiriwa (Gal. 6:13), jambo linalowadhihirisha wao kuwa ni Mataifa wasiotahiriwa. Kama tutakavyoona, Gal. 6:13 hurejea kwa Wanoministi (wapinga-sheria), ambao yawezekana walitaka kufanya tendo la kipagani la kujikata nafsi. Hata hivyo tunapendekeza kufuata mawazo ya Lütgert, kwamba Wana-Uyahudi walikuwa Wayahudi, msimamo wa wana theolojia hawa watatu hauathiri hoja za kitabu hiki.

11. Ragnar Bring, *Der Brief des Paulus an die Galater (Berlin*: Lutherisches Verlagshaus, 1968).

12. Schirrmacher, *Römerbrief 1+2*, *Ethik 1+2.*

13. Nimeondoa pia mjadala juu ya maswali ya kawaida ya utangulizi. Ninakubaliana na Helge Stadelmann, "Die Vorgeschichte des Galaterbriefes"' *Bibel und Gemeinde* 82 (1982) 2: kr. 153-165 na James M. Scott, *Paul and the Nations; The Old Testament and Jewish Background of Paul's mission to the Nations with Special Reference to the Destination of Galatians*,Wissenschaftliche Untersuchungen zum Neuen Testament 84, (Tubingen; J. C. B. Mohr, 1995), kwamba waraka uliandikwa katika mwaka 49 B.K. kwa makanisa ya kusini mwa Galatia ambayo Paulo alikuwa ameyaanzisha wakati wa safari yake ya kwanza ya umisionari (Tazama Stadelmann juu ya hoja ziitwazo Nadharia ya Kusini mwa Galatia na upingaji wa kile kiitwacho Nadharia ya Kaskazini mwa Galatia).

14. C. S. Lewis, *Mere Christianity*, (New York; The Macmillan Company, 1952), uk. 160.

15. Tazama Schirrmacher, *Paulus im Kampf* na Schirrmacher, *Ethik 1*, kr.575-596.

16. Lütgert, *Gesetz und Geist*, uk. 9

17. Rud., kr. 9-11.

18. Rud., uk. 11.

19. Tazama maelezo hapo chini.

20. Lütgert, *Gesetz und Geist, uk.* 11.

21. Theodor Zahn, *Der Brief des Paulus an die Galater*, (1922; kurudiwa kuchapwa. Wuppertal, Germany: r. Brockhaus, 1990) uk. 250.

22. Rud. kr. 1-9.

23. Lütgert. *Gesetz und Geist,* kr 12-13.

24. Theodor Zahn, *Der Brief des Paulus an die Galater* op. cit., uk. 25. Lütgert anarejea kwa Zahn katika *Gesetz und Geist*, kr. 13-14.

25. Tazama Schirrmacher, *Römerbrief* 2, kr.263-284, na Ethik 1, kr. 560-596.

26. Lütgert. *Gesetz und Geist,* kr 15-16.

27. Usiwachanganye na Watheonomisti. Tazama dokezo linalofuata.

28. Neno hili lilianza wakati wa Matengenezo (Tazama Schirrmacher. Ethik 1, kr.607 na 753). Linganisha na neno, 'utawala binafsi au –enye kujiendesha yenyewe' (autonomy), ambalo linatokana na neno la Kigriki 'autos' = 'nafsi' na 'nomos' = 'Sheria' = na hivyo kumaanisha 'sheria ya mtu binafsi'. Neno, 'theonomy' (kutoka katika Kigriki 'theos' = Mungu na 'nomos' = Sheria) huelezea mtazamo kwamba sheria ya maadili ya Agano la Kale, ikijumuisha taratibu za adhabu na siasa, bado ni zenye thamani.

29. Tazama maelezo juu ya Warumi na Wakorintho.

30. Tazama Schirrmacher, *Ethik 1*, kr. 642-655 kwa mjadala kamili zaidi; Schirrmacher. *Römerbrief* 1, kr. 229-236, 252-259.

31. Lütgert, *Gesetz und Geist*, kr. 89-93.

32. Rud., uk. 92.

33. Rud., uk. 42-52

34. Rud., uk. 42

35. Rud., uk. 43

36. Linganisha Rud., uk. 46-47

37. Rud., uk. 47-52

38. Rud., uk. 49

39. Rud., uk. 49-50

40. Rud., uk. 52-57

41. Rud., uk. 55

42. Rud., uk. 57-58

43. Theodor Zahn., op. cit., uk. 120-137.

44. Lütgert, *Gesetz und Geist*, kr. 35-42.

45. Rud., uk. 36.

46. Rud., kr. 36-37.

47. Rud., uk. 61.

48. Rud., kr. 59-62.

49. Daniel C. Arichea na Eugene A. Nida, *A Translators Handbook on Paul's Letters to the Galatians* (London: United Bible Society, 1976) uk. 69.

50. Linganisha Greg L. Bahnsen, *Theonomy in Christian Ethics* (Phillipsburgh, N, J. :Presbyterian & Reformed, 1984) kr. 499, 503-507, 510-517.

51. Rud., kr. 504-505.

52. Linganisha Schirrmacher, *Römerbrief* 1, uk.201-205.

53. Ragnar Bring, "Die Gerechtigkeit Gottes und das alttestamentliche Gesetz:Eine Untersuchung von Rom 10,4", *Christus und das Gesetz: Die Bedeutung des Gesetzs des Alten Testamentes nach Paulus und sein Glaube an Christus,* (Leiden: E. J. Brill, 1969), kr. 59-62. Ragnar Bring. *Der Brief des Paulus an die Galater,* op. cit., kr. 101-166. Baada ya Bring, uchunguzi bora wa Wagalatia 3 *ufahamikao kwangu ni kile kiambatisho cha* Greg. L. Bahnsen. *Theonomy in Christian Ethics,* op. cit., kr 499-515, na katika C. E. B. Cranfield. "St. Paul and the Law", *Scottish Journal of Theology* 17, 1967, kr. 43-64, na katika Wilhelm Lütgert, *Gesetz und Geist.*

54. Tazama Schirrmacher. *Römerbrief,* op. cit., kr. 132-137 na Schirrmacher. Ethik, op. cit., kr. 17-22, kwa mjadala kamilifu.

55. *C. E. B. Cranfield. A critical and Exegetical Commentary on the Epistle to the Romans, Vol. 2,* The International Critical Commentary 11, (Edinburg: T & T Clark, 1989), kr.519. Tazama

mjadala kwenye kurasa 515-519, na Cranfield's "St. Paul and the Law", op. cit., kr. 48-49.

56. Felix Fluckiger. "Christus, des Gesetzes telos", *Theologische, Zeitschrift*, 11, Basel, 1955, kr. 153-157.

57. Rud.

58. Rud., uk. 155.

59. Rud.

60. Tafsiri hii ya Warumi 10:5 inakubaliwa pia na C. E. B. Cranfield katika Kitabu chake, *A Critical and Exegetical Commentary on the Epistle to the Romans,* op.cit., Vol. 2, kr. 520-522, na katika kitabu chake "St. Paul and the Law", op. cit., kr. 48-53. Pia tazama Walter C. Kaiser, "The Weightier and Lightier Matters of the Law", katika kitabu cha Gerald F. Hawthorne (ed.). *Current Issues in Biblical and Patrisitic Interpretation,* (Grand Rapids, Mich.: Wm. B. Eerdmans, 1975), kr. 176-192; Walter C. Kaiser, "Leviticus 18:5 and Paul: Do this and You Shall Live (Eternally?)", *Journal of the Evangelical Theological Society* 14 (1971) kr.19-28; *Fuller, Unity,* kr.462-471.Mtazamo wa Kilutheri unawasilishwa na Peter von Osten-Sacken, *Die Heiligkeit der Thora* (Munich: Chr. Kaiser, 1989) kr. 33-43, na kutetewa na Daniel P. Fuller. Gospel and Law; Contrast or Continuum? (Grand Rapids, Mich.: Wm. B. Eerdmans, 1980) kr. 66-68; Ragnar Bring. "Die Gerechtigkeit Gottes und das *Alttestmentliche Gesetz*: Eine Untersuchung von Rom 10, 4", op. cit., Ragnar Bribg. *Christus und das Gesetz*, op. cit., Ragnar Bring. Der Brief des Paulus an die Galater, op. cit. Ragnar Bring. "Luthers Lehre von Gesetz und Evangelium als der Beitrag der lutherischen Theologie fur die Okomene", katika kitabu cha Ernst Kinder, Klaus Haendler (ed.). *Gesetz und Evangelium,* Wege der Forschung CXLII, (Darmstadt: Wissenschaftliche Buchgesellschaft, 1986), kr. 76-123.

61. Tazama mjadala katika Schirrmacher, *Ethik 2*, kr.20-22.

62. Walter C. Kaiser, "Leviticus 18:4 and Paul", op. cit.; Walter C. Kaiser, *Towards an Old Testament Theology* (Grand Rapids, Mich.: Zondervan, 1978) kr. 110-115.

63. Rud., uk. 115.

64. Mfano, mpaka wa maana ulifikiriwa lakini haukuelezwa.

65. Daniel C. Arichea na Eugene A. Nida, po. Cit., uk. 62.

66. Tazama mjadala bora wa maelezo haya katika kitabu cha Wagalatia katika Daniel P. Fuller, "Paul and the 'Works of the Law'", *Westminster Theological Journal 38, 1975-76, kr. 28-42; Fuller, Unity,* p. 471-477, na Brice L. Martin, Christ and the Law in Paul, Supplement to Novum Testmentum 62, E. J. Brill, (Leiden, 1989) kr. 24-25.

67. Juu ya maelezo, 'matendo', tazama Schirrmacher, *Ethik 2*, kr.5-10, na *Römerbrief 1*, Kr. 206-210.

68. Theodore H. Epp, *Galatians* (Lincoln. Nebraska: Back to the Bible Correspondence School, 1974) uk. 334.

69. Ragnar Bring, *Der Brief des Paulus an die Galater*, uk. 177.

70. Tazama tafsiri fupi ya Luther ya 1519 n1 1523 katika *Martin Luthers Samtliche Schriften*, Vol. 8, Col 1351661 (ed Joh. Gerg Walch) 23 Volumes (1910, rep. Grob Oesingen, Germany: Verlag der Lutherischen Buchhandlung H. Harms, 1986); toleo refu la 1535 katika kitabu kile kile, Vol. 9, Col. 1-797; mahubiri ya 1532 juu ya Wagalatia 3:23-24, Rud., Vol, Col. 798-811.

71. Rud., Vol. 9, Col. 807.

72. Lütgert, *Gesetz und Geist,* uk. 69.

73. Ragnar Bring, *Der Brief des Paulus an die Galater*, uk. 167.

74. Wilhelm Lütgert, *Schopfung und Offenbarung*, (Giessen, Germany: Brunen Verlag:1984), uk.279.

75. Tazama Lütgert, *Gesetz und Geist.*

76. Tazama Lütgert, *Gesetz und Geist* na Schirrmacher, *Ethik 2*, kr. 48-77.

77. Lütgert, *Gesetz und Geist,* kr. 61-64.

78. Lütgert, *Gesetz und Geist,* kr. 63-64.

79. C. E. B. Cranfield, "St. Paul and tha Law', kr. 61-62.

80. Sptuaginta iliwatambua "makumi elfu ya watakatifu" (Kum. 33:2) waliohudhuria utoaji wa Sheria katika mlima Sinai kuwa ni malaika. Tazama Rud., kr. 61-62.

81. Ragnar Bring, *Der Brief des Paulus an die Galater,* kr. 144-146.

82. Herman Witsius, *The Economy of the Covenants between God and Men: Comprehending A Complete Body of Divinity,* Vol. 2(Escondido, Cal.: The den Dulk Christia Foundation) na (Phillipsburg, N. J.: Presbyterian and Reformed, 1990) uk. 163.

83. Thomas Schirrmacher,, “Der trinitarische Gottesglaube und die monotheitischen Religionen”, katika Rolf Hille na Eberhard Troeger (ed.) *Die Einzigartigkeit Jesu Christ*, TVG (Wuppertal, Germany: Brockhaus Verlag., 1993) kr. 113-151, juu ya masomo ya Kristo na Malaika wa BWANA katika Agano la Kale. Pia tazama Thomas Schirrmacher, “Trinity in the Old Testament and Dialogue with the Jews and Muslims”, *Calvinism Today 1*(1991) Iliyorudiwa kuchapwa katika *Field Updated: GR International*, April/May 1991, kr. 6-8 na June/July 1991, kr. 5-8.

84. Herman Witsius *The Economy of the Covenants between God* and Men: op. cit., Vol 2, uk.163; Carl F. Keil. *Genesis und Exodus* (Giessen, Germany: Brunnen Verlag, 1983) kr. 503-504. Dokezo la 2 linachukua nukuu ya Ernst Wilhelm Hengstenberg “Christogie des Alten Testamentes” yenye tamko kuwa Sheria ilitolewa na malaika, lakini katika uchunguzi wa mwisho, ilitolewa na Mungu na Kristo.

85. John Calvin, *Unterricht in der chrislichen Religion: Institutio Religionis Christianae,* Vo. 2, (Neukirchen, Germany: Neukirchener Verlag, 1983), kr. 260-284 (kitabu cha 2, sura ya 11mpaka ya 12); Heinrich Berger, *Calvins Geschichtsauffasung*: *Studien zur Dogmengeschichte und Systematischen Theologie 6,* (Zurich: Zwingli Verlag, 1956), kr. 99-100.

86. Hermann Witsius, op. cit., Vol. 2, uk. 367.

87. Herman N. Ridderbos, T*he Epistle of Paul to the Churches of Galatia* (Grand Rapids, Mich.: Wm. B. Eerdmans, 1953) uk.146.

88. Schirrmacher, *Ethik* 1, kr.691-700; *Römerbrief 2*, kr. 26-50 na N. J. Lund, “Law, Threefold Use of the”, katika R. K. Harrison (ed.), Encyclopedia of *Biblical and Christian Ethics*, (Nashville: Thomas Nelson, 1987), kr. 226-227.

89. Katika histilahi ya Kilatini, tazama Horst Georg Pohlmann, *Abri der Dogmatik* (Gutersloh, Gutersloher Verlagshaus:1980) kr. 40-41.

90. Rud. uk. 41.

91. Utendaji kazi wa dhamiri.

92. C. E. B. Cranfield, “St. Paul and the Law”, op. cit., uk. 63.

93. Lütgert, *Gesetz und Geist,* kr. 71-83.

94. Rud. uk. 80.

95. Rud. kr. 71-83; sawasawa na Ragnar Bring, *Der Brief des Paulus an die Galater,* op. cit., kr. 181-182.

96. Lütgert, *Gesetz und Geist,* uk. 168.

97. Lütgert, *Gesetz und Geist,* uk. 78.

98. Georg Huntemann, *Der verlorene Ma stab :Gottes Gebot im Chaos Dieser Zeit* (Bad Liebenzell, Germany: VLM, 1983), kr. 33.

99. Tazama Lütgert, *Gesetz und Geist*, kr. 83-88.

100. Rud. uk. 87.

101. John Calvin, Galaterbrief, op. cit., uk. 69.

102. Lütgert, *Gesetz und Geist*, uk. 88.

103. David Chilton, *Productive Christians in an Age of Guilt-Manipulators: A Biblical Response to Ronald J. Sider* (1985, rep. Tyler, Texas: ICE, 1986), uk.76. Tazama kr. 69-76 juu ya Amri Kumi.

104. Georg Huntemann, *Der verlorene Ma stab*, op. cit., uk. 24.

105. Pinchas Lapide, *Die Bergpredigt: Utopie oder Programm?* (Mainz, Germany: Matthias-Grunewald-Verlag, 1992) uk.22.

106. George Downame, *The Christians Freedom (The Doctrine of Christian Libetry)* (Oxford, 1935; rep. Pittsburg:Soli Deo Gloria Publ., 1994), uk. 69.

107. Tazama Schirrmacher, *Ethik* 1, kr. 685-690 na 801-846, vilevile Schirmacher, *Römerbrief* 1, kr. 183-188 kwa hoja zilizosheheni.

108. Katika Gal. 5:6, imani itendayo kwa upendo huchukua nafsi ya amri. Paulo anamaanisha kitu kile kile, kwa kuwa wazo la Kibiblia la “Upendo” halijumuishi kamwe maneno au hisia tu, bali linaelezewa katika vitendo vinavyokubaliana na sheria ya upendo, kanuni iongozayo ya amri zote na Sheria kamili.

109. Tazama Scirrmacher, *Ethik* 2, kr. 82-145 juu ya Hotuba Mlimani.

110. Christoph Haufe, *Die sittliche Rechtfergtigung des Paulus* (Halle, Germany: Max Niemeyer, 1957) kr. 20-30, anajadili juu ya mtazamo wa Paulo kibiblia wa Kuhesabiwa haki. Tazama pia Walter C. Kaiser, The

Weightier and Lightier Matters of the Law", op. cit.; na Brice L. Martin, ed. *Christ and the Law*, op. cit., 32-34.

111. Tazama Schirrmacher, *Römerbrief 2*, uk. 22 kk na *Ethik* 1, kr. 677-684 na 191-192, vilevile kurasa zilizonukuliwa hapo juu, juu ya sheria ya maadili na ile ya maadhimisho.

112. Tazama Schirrmacher, *Ethik* 1 and 2, na Schirrmacher, *Römerbrief* 2 juu ya sheria ya maadili na ile ya maadhimisho.

113. Aurelius Augustinus, 'Brief an Hieronymus' iliyonukuliwa katika : Alfons Heilmann, ed., *Texte der Kirchenväter,* Vol. 2 (Munich: Kosel, 1963) uk.440. (iliyotafsiriwa kutoka kijerumani). Augustine alidhani kwamba sheria ya maadhimisho ingekufa taratibu.

114. Lütgert, *Gesetz und Geist,* kr. 34-35.

115. Tazama: Fuller, *Unity*, kr. 459-480; William Hendriksen, *Galatians and Ephesians, in New Testament Commentary* (1969, repr. Edinburg: The Bunner of Truth Trust, 1990.); H. H. Schmitz, *Paulus schreibt an die Galater* (Hamburg: Advent-Verlag, 1971, kr. 180-182 {kutoka katika mtazamo wa kiadventista})na waandishi wa kiprotestanti na wa kiyahudi wametajwa hapa.

116. Tazama Merril C. Tenney, *Galatians: The Charter of Christian* Liberty (1950, repr. Grand Rapids: Wm B. Eerdmans, 1986), uk. 155 kwa ajili ya utambulisho mzuri wa matumizi ya neno, 'sheria' katika Wagalatia. Tenney hashirikiani na mtazamo wangu wa Waraka kwa Wagalatia.

117. Christoph Haufe, *Die sittliche Rechtfergtigung des Paulus,* op. cit., kr. 20-30.

118. C. E. B. Cranfield, "St. Paul and the Law", op. cit., kr. 63-64.

119. Christoph Haufe, *Die sittliche Rechtfergtigung des Paulus*, op. cit., kr. 22. Ninatafsiri kifungu hiki kwa hali tofauti kidogo, lakini hiyo hailegezi thamani ya tamko la Haufe.

120. Lütgert, *Gesetz und Geist,* kr. 27-34.

121. Rud. kr. 30-31.

122. Rud. uk. 32

123. Rud. uk. 33

124. Rud. uk. 33

125. Rud. uk. 34

126. Kwa kuwa kifungu hiki katika Kigriki hakina vituo (alama za kimaandishi) fikirio hilo sio tu kwamba lawezekana, bali pia ni muhimu.

127. Lütgert, *Gesetz und Geist,* kr. 22-27.

128. Rud., uk. 23.

129. Rud., uk. 24.

130. Rud., uk. 27

131. Rud., kr. 96-106.

132. Rud., uk. uk. 97.

133. Rud., uk. uk. 97.

134. Rud., uk. 98.

135. *The Westminster Confession of Faith,* (Galasgow: Free Presbyterian Publications: n.y.), uk. 87.

136. Lütgert, *Gesetz und Geist*, uk. 17.

137. Rud., uk. 18.

138. Rud., uk. 19.

139. Hata kama mstari wa 23 unawaelekea Wana-Uyahudi, si muhimu kuwa unakanusha uhalali wa Sheria, kama ambavyo tafsiri ya John Calvin inavyoonesha. “Sheria haikomi kufanya wajibu wake wa kufundisha na kusihi, lakini Roho wa Uana hutukomboa kutoka katika kongwa lake.” Johannes Calvin, Auslegung der Heiligen Schrift in deutscher Ubersetung : Der Galaterbrief (Neukirchen, Germany: Buchhand lung des Erzei hungsvereins, n.d.) uk. 92.

140. Lütgert, *Gesetz und Geist,* uk. 61.

141. Rud., uk. 20.

142. Gerhard Friedrich, “Das Gesetz des Glaubens Rom 3:27”, *Theologische Zeitschrift* 10 (Basel; 1954) kr. 401-407; Hermann Cremer, Julius Kogel, *Biblisch-Theologisches Worterbuch des neutestament lichen Griechisch* (1915, Stuttgart: f. A. Perthes, 1923) anashirikiana mtazamo huu, kama afanyavyo Peter von Osten-Sacken, *Die Heiligkeit der Thora,* op. cit., kr. 23-33; na C. E. B. Cranfield, A Critical and *Exegetical Commentary on The Epistle to the Romans,* Vol. 1, op. cit., kr. 219-220.

143. Peter von Sacken, Rud., kr. 14-42, anayaona maelezo haya kuwa rejea kwa Torati (kwa Sheria) iliyoeleweka vema. Brice L. Martin, *Christ and the Law in Paul,* op. cit., kr. 26-32, anajadili wawakilishi wengine wa msimamo huu.

144. Clement of Alexandria, ‘Der Erzieher’, 1.9 ananukuliwa na Alfons Heilman, Ed., *Texte der Kirchenvater,* Vol. 2 (Munich: Kosel, 1963) uk. 149.

145. Christoph Haufe, *Die sittliche Rechtfergtigung des Paulus*, op. cit., uk. 11.

146. Schirmaccher, *Römerbrief* 2, kr. 242-262 na Ethik 1, kr. 189-214.

147. Eckard J, Schnabel, *Law and Wisdom from Ben Sira to Paul* (Tubingen, Germany: J. C. Mohr, 1985) uk. 297- nukuu zimetafsirwa kutoka Kigriki na Kilatini. Tazama pia C. E. B. Cranfield, "St. Paul and the Law op. cit.

148. Lütgert, *Gesetz und Geist*, uk. 20.

149. Thomas Schirrmacher, "Der Mythos von der Gestzlichkeit", *Fundamentum* (1993) 3, kr. 39-43.

150. Gordon H. Clark, "Legalism", *Baker's Dictionary of Christian Ethics.* Ed. Carl. F. Henry (Grand Rapids, Mich: Baker Book House, 1973), uk. 385; iliyochapwa kwa mara nyingine na Gordon H. Clark katika, *Essays on Ethics and Politics* (Jefferson, MD: Trinity Foundation, 1992), uk. 150.

151. Rud.

152. Greg L. Bahnsen, By This Standard: *The Authority of God's Law Today* (Tyler, Tex.:ICE, 1985), kr. 76-68.

153. Alfred de Ouervain, *Die Heiligung, Ethik,* Part 1 (Zollikon: Evangelischer Verlag, 1946), uk. 259.

154. Schirrmacher, *Ethik,* Vol. 1, kr. 297-304 *juu ya Brunner* (kr. 292-306); Thomas Schirrmacher, *Das Mi verstandinis des Emil Brunner: Emil Brunner's Bibliologie als Ursache fur das Scheitern seiner Ekklesiologie*, Theologische Untersuchungen zu Weltmission und Gemein debau, ed. Hans-Georg Wunch und Thomas Schirrmacher (Lorrach, Germany: Arbeitsgemeinschaft fur Weltimission und Gemeindebau, 1982); Thomas Schirrmacher, "Das Mi verstandnis der Kirche und das Mi verstandnis des Emil Brunner", *Bibel und Gemeinde* 89 (1989), kr. 279-311.

155. Emil Brunner, *Das Gebot und die Ordnungen* (Zurich: Zwingli Verlag, 1939), uk.79.

156. Tazama pia Robertson McQuillkin, *An Introduction to Biblical Ethics* (Wheaton, III.: Tyndale House Publ., 1989); David Chilton, *Productive Christians in an Age of Guilt-Manipulators*, op. cit., kr. 22-25, anaorodhesha aina nne za ushika sheria; 1. Kuhesabiwa haki kwa matendo; 2. Kuifanya sheria ya maadhimisho kuwa lazima; 3. Kuzifanya sheria zilizotungwa na binadamu kuwa lazima; 4. Mkanganyo wa dhambi na uvunjaji wa sheria unaotendewa kazi na Serikali.

157. Eduard Bohl, Dogmatik: *Darstellung der christlichen Glaubenslehre auf reformiert – kirchlicher Grundlage* (Amsterdam: Scheffer, 1887), uk. 515.

158. Rud., maelezo mafupi 1, uk. 515.

159. Imechukuliwa kutoka Schirrmacher, *Römerbrief* 1, kr. 38-39 na Thomas Schirrmacher, *Der Text des Römerbriefes fur das Selbsstudium gegliedert – mit Tabellen und Ubersichten* (Bonn: Verlag fur Kultur und Winssenschaft, 1994), kr. 10-11.

160. Mbali na kazi zake juu ya Wagalatia na Warumi, tazama; Lütgert, *Freiheitspredigt und Schwarmgeister in Korinth*, Beiträge zur Forderung christlicher Theologie 12, Vol. 3 (1908) (Gutersloh, Germany: C. Bertelsmann, 1908), kr. 136-157 juu ya Warumi, Wafilipi na Wagalatia, na kitabu chote juu ya Wakorintho; Wilhelm Lütgert, *Amt und Geist im Kampf, Studien zur Geschichte des Urchristentums,* Beiträge zur Forderung christlicher Theologie 15, Vol. 4/5 (1911) (Gutersloh, Germany: C. Bertelsmann, 1911). Tazama pia Wilhelm Lütgert, *Die Liebe im Neuen Testament* (Leipzig: A. Deichert, 1905, repr. Giessen, Germany: Brunnen Verlag, 1986).

161. Lütgert, *Römerbrief.*

162. Schirrmacher, Römerbrief 1, kr. 32-44, *Römerbrief* 2, kr. 148-150 na komentari kamili ya Warumi.

163. Otto Michel, *Der Brief an die Romer,* Kritisch-exegetischer Kommentar uber das Neue Testament 414 (Gottingen, Germany: Vanden hoeck & Ruprecht, 1978), uk. 40.

164. Lütgert, *Römerbrief,* kr. 111-112.

165. Rud., kr. 69-79.

166. Rud., kr. 79-90.

167. Ray R, Sutton, “Does Israel have a Future?”, *Covenant Renewal* 2 (Tyler, Texas: 1988) 12 (Dec.) 1-4.

168. Ray R. Sutton, *That you may Prosper: Dominion by Covenant* (Tyler, Texas: ICE, 1987), kr. 246-252: Sutton anajadili zaidi, mitindo migumu kabisa ya Agano katika Warumi. Mtindo wa Agano katika Agano la Kale ambao unagongana sawasawa na ule a mikataba ya Mashariki ya Kati, huanza na ombi kwa Mungu na maelezo juu yake (avukaye mpaka au aliye bora sana), huelezea utegemezi (ngazi), masharti ya agano (maadili), hitimisho (kiapo) na huonesha ni kwa umbali gani agano huvifunga vizazi (urithi). Schirrmacher, Ethik 1, kr. 351-394 hutoa maelezo zaidi.

169. Maelezo ya Paulo, ‘Hasha’ yanafanana na maelezo ya Agano la Kale ‘Ipishilie mbali’ na viapo vingine, na kimsingi hutumika katika Warumi na katika Wagalatia: Rum. 3:4, 6, 31; 6:2, 15; 7:7, 13; 9:14; 11:1; 1 Kor. 6:15; Gal. 2:17; 3:21; 6:14 (hapa kukiwa na nyongeza ‘lakini mimi’). Septuaginta inatafsiri neno la Kiebrania kiapo, ‘ipishilie mbali’ kwa maneno ‘me geneito’ katika Mwa. 44:7, 17; Yos. 22:29; na 1 Fal. 21:3 (LXX 20;3) vinginevyo hutafsiri kwa neno ‘medamos’ au ‘sivyo kabisa’. Septuaginta hutafsiri ‘amen’ kwa maneno ‘geneito, geneito’ katika Zab. 72:19 (LXX 71:19). Maelezo ya Agano la Kale, ‘ipishilie mbali’ inachukuliwa kutoka katika maelezo ‘to desecrate – kukufuru) na humaanisha ‘Na nijinajisi mbele za Mungu ikiwa…” (Georg Giesen, *Die Wurzel sb’, “schworen”: Eine semasiolligsche Studie zu Eid im Alten Testament*, Bonner Biblische Beiträge, Konigstein: Peter Hanstein, 1981, uk. 43). Tazama Schirmmacher, *Ethik* 2, kr. 129-133 na 115-145.

170. Kigriki/Kiyunani, ‘me genoito’.

Maelezo ya Maneno

Komentari: Kitabu kinachohusika na hoja, maoni, maelezo au mafafanuzi zaidi juu ya kile kinachosemwa au kilichoandikwa. Kwa hiyo Komenteta ni mwandishi au mtoa hoja, maelezo au mafafanuzi zaidi.

Muktadha: Maelezo yaliyotangulia na yanayofuata kifungu husika yanayodokeza mazingira ya kifungu hicho.

Istilahi: Msamiati maalumu utumikao katika shughuli Mahususi (mfano, istilahi ya kitheolojia “Utatu”; istilahi ya kibenki “hawala ya fedha”).

Uliberali: Mtazamo wa kimageuzi au uendao kinyume na hali ya kawaida iliyozoeleka na kukubalika

Dhamira: Jumla ya mawazo yote ya mwandishi; hivyo, dhamira kuu ni wazo kuu la mwandishi linalotawala kazi (maandishi) yake.

Hadhira: Wasomaji au wasikilizaji.

Kishazi: Tungo yenye kitenzi (kitendo) ndani yake.

Mchakato: Hatua mbalimbali katika utekelezaji wa jambo fulani.

Wanasilia: Watu washikiliao misingi ya awali kabisa (fundamentalists).

Udogma: Mfumo wa imani uliowekwa upaswao kufuatwa bila kuulizwa au kutiliwa mashaka.

Matengenezo: Wakati kanisa lilipokabiliana na mageuzi makubwa yaliyolenga kulirudisha kwenye misingi ya Biblia (reformation).

Amali: Jumla ya mambo yote kwenye jamii yanayoenziwa na kuthaminiwa.

Uzamo/Upayatisti: Hali ya kujitoa kabisa kwa Mungu (Pietism).

Vifupisho vya Maneno

- kk. - kuendelea
- kr. - kurasa
- k.v – kama vile
- Rud. – rudia kitabu kilichotajwa hapo juu
- uk. - ukurasa

Mwandishi

Thomas Schirrmacher ni mwenyekiti wa Theolojia ya Elimu-maadili (ethics), Umisheni (missions) na Dini za ki-Ulimwengu (world religions), ni Rais wa Martin Bucer Theological Serminary na Rais wa Gebende Hande gGmbH (Giving Hands: 'Mikono Itoayo') ambalo ni shirika hai la kimataifa la misaada; na vile vile mmiliki wa shirika la uchapaji (Publishing House) na mmiliki mdau wa shirika la ushauri (Consulting Company).

Schirrmacher alizaliwa mwaka 1960, alisoma theolojia kuanzia mwaka 1978 hadi 1982 huko STH Basel na tangu mwaka 1983 alisomea Elimu ya Utamaduni wa Binadamu (Cultural Anthropology) na Ulinganifu wa Dini (Comparative Religions) katika Bonn State University. Alitunukiwa Shahada ya Uzamivu wa theolojia katika umisheni (Drs. Theolgy in Missiology) huko Johannes Calvin Foundation (Kampen/Netherlands) mwaka 1985, Shahada ya Uzamivu wa Falsafa katika Elimu ya utamaduni wa binadamu (Ph.D in Cultural Anthropology) huko Pacific Western University, Los Angeles (CA) mwaka 1989 na Shahada ya Uzamivu wa Theolojia katika Elimu-maadili (Th. Din Ethics) huko Whitefield Theological Seminary, Lakeland (FL) mwaka 1996. Katika mwaka 1997 alitunukiwa shahada ya heshima ya Uzamivu (D.D) kutoka Cranmer Theological House.

Alikuwa mchungaji wa Jamii ya Kiinjili ya Ujerumani (Evangelical Society of Germany) huko Bonn na Erftstadt mwaka 1982 hadi 1986, mchungaji mdau wa Kanisa Huru la Kiinjili (Evangelical Free Church) huko Bonn mwaka 1992 hadi 1998 na mchungaji wa Free Reformed Church huko Bonn mwaka 1998 hadi 2000.

Schirrmacher alifundisha Umisheni Dini za ki-Ulimwengu na Elimu ya utamaduni wa Binadamu huko FTA Giessen (Germany) kutoka mwaka 1983 hadi 1989, na kutoka mwaka 1990-1996 alifundisha Elimu ya maadili, misheni, ulinganifu wa Dini, na Elimu ya utamaduni wa Binadamu huko 'Independent Theological Seminary' mjini Basel ('Staatsunabhangige Theologische Hochschule Basel'-STH Basel). Alishikilia na anashikilia viti mbali mbali vya uprofesa, kwa mfano 1994-1999 'Philadelphia Theological Seminary' (PA, USA) (Umisheni), 1995-2000 huko Cranmer Theological House (Shreveport, LA) (umisheni na Elimu-maadili), na tangu 1996 huko Whitefield Theological

Seminary (Lakeland, FL), (Systematic Theology-Theolojia pangilivu na Apologetics-utetezi-imani). Hutoa mihadhara au hufanya kazi katika mashule mbalimbali kama Freie Theologische Academie (Giessen, Systematic Theology), The Neues Leben Seminar (Altenkirchen, Systematic Theology), the Academie fur Christliche Fuhrungskrafte (Grummersbach, Bussiness Ethics) na UNISA (University of South Africa).

Mbali na hayo anajihusisha sana kimataifa na elimu (postgraduate) ya masafa (distance) na tovuti (internet education), mfano, yeye ni mhusika mkuu wa Elimu ya Kitheolojia ya Ujerumani (Germany Theological Education) kwa njia Enezi (Extension) ('Theologischer Fernunterricht des Neues Leben-Seminars' au the European Extension of Whitefield Theological Seminary). Pia anahusika katika shughuli zote mbalimbali za uchapaji. Amekuwa mhariri wa "Bibel und Germeinde' kwa miaka kumi, sasa ni mhariri wa 'Evangelikale Missiologie', mhariri mdau wa 'Contra Mundum: A Reformed Cultural Review', mhariri wa 'Reflection: An International Reformed Review of Missiology' na Querschnitte. Ameandika na kuhariri vitabu 49 juu ya Elimu-maadili misheni na Elimu ya utamaduni wa Binadamu.

Tangu 1986 anamiliki shirika la uchapaji la 'Cultural and Science Publ.' (Verlag fur Kultur und Winnsenschaft), ambalo huchapa vitabu vya kisayansi juu ya lugha, desturi, dini na umisheni. Ni mmiliki mdau wa Consulting Schirrmacher GbR, shirika la kibiashara na biashara ya elimu (Business and Educational Business company).

Anatajwa katika Marquis "Who's Who in the World", katika "International Who is Who of Professionals", katika "Who is Who in der Bundes republik Deustchland" na katika "International Who's Who in Distance Learning".

Amemwoa mtaalamu wa Uislamu Dr. Christine Schirrmacher, Mkurugenzi wa Islam Insitute of the Lausanne Movement, Germany. Ni profesa azungukaye wa Masomo ya Uislamu huko "Whitefield Theological Seminary (USA), na mwandishi wa vitabu viwili bora vya Utambulishi wa Uislamu. Wana ndoa hawa wana watoto wawili wadogo.

Vitabu vya Kiingereza vya Dk. Thomas Schirrmacher

Legends about the Galileo-Affair

Kitabu hiki kinalenga msingi wa kweli wa kihistoria wa suala la Galileo. Kwa nyongeza kinajumuisha mchango zaidi wa mwandishi katika utafiti wa uumbaji, hususani habari ya uumbaji katika kitabu cha Mwanzo na athari za mawazo ya mabadiliko (evolution) katika maadili na historia ya kitamaduni.

ISBN 3.928936-21-2, Pb. 120 p. DM 16,80

GOD Wants YOU to Learn, Labour and Love

Kijitabu hiki kinajumuisha makusanyo ya insha hususani zilizopangwa na mwandishi kuwatia moyo na hamasa watu ambao wanajihusisha na kazi ya misheni.

ISBN 3-928936-17-4, Pb. 64 p. DM 5,90

World Mission-Heart of Christianity

Mmoja kati ya maprofesa wa kiinjili wa misheni wanaoongoza na mwanaharakati wa huduma ya misheni nchini Ujerumani aonesha katika njia ya kushangaza, jinsi asili ya Mungu, ya Biblia na Imani ya Kikristo ilivyo kiini cha huduma ya misheni duniani.

Human Rights Threatened in Europe

Utoaji mada kwenye Kusanyiko la Kwanza la Ulaya juu ya mhadhara wa Tetea-Uhai huko Berlin ukijihusisha na Utoaji mimba, Uondoaji wa uhai kwa hiari, Kusanyiko juu ya Baolojia-maadili (Bioethics-Convetion) n.k.

Law or Spirit?

Kwa mtume Paulo ushika-sheria na ukosa-sheria yalikuwa ni makosa yenye kuhuzunisha yaliyo sawa. Roho Mtakatifu humwongoza mwamini katika uelewa sawia juu ya Sheria ya Mungu iliyofunuliwa [Kiswahili: Sheria au Roho?].

ISBN 3-929836-22-0, Pb. 86 p. DM 12, 80